
SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**TMA** yahadharisha mvua kubwa kunyesha Dar na Kanda ya Ziwa

UKURASA 3



**BAYERN HAWAMTAKI HAALAND**

UKURASA 22


# Nipashe

Jumatano Desemba 29, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579809

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper


# Samia: Mikopo lazima

**Asisitiza** lengo ni kupata fedha miradi mikubwa, mkataba awamu ya tatu SGR rasmi... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan, akishuhudia utiaji saini mkataba wa mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kipande cha Makutupora -Tabora chenye urefu wa kilometa 368 awamu ya tatu (Lot III). Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, akitia saini mkataba huo na Makamu Mwenyekiti wa Kampuni ya Yapi Merkez ya Uturuki, Erdem Arioglu, Ikulu jijini Dar es Salaam, jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

## YALIYOMO


UKURASA WA 3
**UAMUZI KESI NDOGO KINA SABAYA LEO**
MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha leo inatarajia kutoa uamuzi wa ama kukataa...

UKURASA WA 5
**IGP SIRRO ASEMA UHALIFU UMEPUNGUA**
MKUU wa Jeshi la Polisi, IGP Simon Sirro, amesema uhalifu nchini kwa kipindi cha miaka...

UKURASA WA 16
**MBARONI TUHUMA MAUAJI KISA KUGOMBEA CHAKULA**
JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linamshikilia kijana mmoja na wengine watatu wanasakwa...


# Waganga tiba asilia mabalozi hamasa chanjo ya corona

UKURASA 3



Mtaalamu wa Ufuatilia na Udhibiti wa Magonjwa kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Baraka Nzobo, akijibu maswali ya wananchi waliotaka kujua kuhusu chanjo ya UVIKO-19 katika kampeni inayoendelea mkoani Singida kuhamasisha utoaji wa chanjo kwa Mpango Shirikishi na Harakishi Awamu ya Pili. (Kushoto) Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Itigi, Dk. Emmanuel Mallange. **PICHA: MARY GEOFREY**

# Wadau wa haki wataka tume uchunguzi kuhojiwa Mwingira

UKURASA 2


Scan Hapa



Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store


**MICHEZO** **CAF YAMRUDISHA CHAMA SIMBA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimwapisha Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Lela Mohammed Mussa, kuwa Mjumbe wa Tume ya Mipango, Ikulu jana. PICHA: IKULU

# Samia asema mikopo lazima

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema serikali yake itaendelea kukopa ili kuhakikisha inakamilisha miradi yake yote iliyoanzishwa na kuanzisha mipya kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya utiaji saini mkataba wa mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kipande cha Makutupora-Tabora awamu ya tatu kinachotarajiwa kugharimu zaidi ya Sh. trilioni nne.

"Kuna watu wameanza kufanya jitihada za kutuvunja moyo kwenye mikopo. Ninataka niwaambie tu kwamba hakuna nchi isiyokopa, hata nchi zilizoendelea zina mikopo mikubwa kuliko ya kwetu. Tutakopa ili tumalize miradi ya maendeleo na ili tuendelee kwa sababu ukikopa unajenga sasa kwa haraka kuharakisha maendeleo, ukisubiri ukusanye za kwako utamaliza lini kujenga? Mradi wa matrilioni, utaumaliza lini? Lakini kopa, tengeneza haraka, nenda kalipe polepole.

"Na wakopeshaji wanakupa muda, miaka 20, ni kujua tu unajadiliana nao vipi kwenye mikopo. Tumekopa mkopo wa masharti nafuu, miaka 20 unakudhuru nini? Lakini maendeleo yanakuja haraka. Kuna mkopo tumekopa na baada ya kuona tumefanya vizuri kwenye maendeleo ya jamii tumeongezwa nyingine na shirika lile lile, tena kwa masharti nafuu, miaka 20 unakosa nini? Unaharakisha maendeleo, unakusanya kidogo unaenda kulipa," alifafanua.

Rais Samia alisema haoni kama kuna jambo baya kwenye kukopa, akisisitiza kuwa kikubwa ni kuzingatia na kusimamia misingi ambayo nchi imejiwekea.

"Hakuna ubaya kwenye hilo, lengo ni kusimamia misingi yetu, kuhakikisha hatubinywi, uchumi wetu unakua, mikopo yetu tunayochukua iwe ni mizuri na uchumi ukue, kila mmoja anufaike. Sasa wale wanaosema mkopo ni kurudi nyuma inategemea na unavyoutumia.

"Hata kwenye kawaida, tunatoa mikopo ya halmashauri ya asilimia 10, kuna wanaochukua wakaitumia 'wakenda' vizuri, na kuna anayechukua akifika nyumbani baba anamwambia 'leta' anakwenda kupiga ulanzi, kazi imekwisha.

"Kwa hiyo, mikopo ni mikopo, hata tukiangalia mikopo hii tuliyochukua ya Sh. trilioni 1.3, nchi ngapi zimechukua? Wametumia kama tulivyotumia Tanzania? Hapana! Kila nchi ilitumia kivyake. Kwa hiyo, usiseme tu mkopo, angalia mkopo unavyotumika halafu ndio useme," alisema.

### MIRADI MIKAKATI

Kuhusu miradi ya kimkakati, Rais Samia alisema wapo baadhi ya watu ambao walikuwa wanasubiri kuona miradi hiyo inakwama ili wapate la kuzungumza, akisisitiza hakuna mradi utakaokwama.

"Kuna mradi wa Bwawa la Nyerere, Daraja la Busisi, sijui miradi ya barabara, sijui reli na mingine yote, hakuna itakayokwama, na niwaambie tu kwamba hakuna mradi hata mmoja ambao tunadaiwa pesa, makandarasi wamekwishalipwa yote, sisi ndio tumebaki tunadai kazi," alisema.

### UJENZI SGR

Mkuu wa nchi huyo alisema ujenzi wa SGR mpaka sasa uwekezaji ni wa Sh. trilioni 14.7 na serikali itahakikisha inatumia mbinu zote ikiwamo kukopa ili kukamilisha miradi ya reli iliyoianzishwa.

Rais Samia alimwagiza Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Hussein Katanga, kuunda timu ya wataalamu ambao watakaa na kuweka malengo ya kusimamia na kuangalia miradi yote ambayo serikali inawekeza ili kuhakikisha inasimamiwa ipasavyo.

"Kama nilivyosema uwekezaji mpaka sasa hivi ni Sh. trilioni 14.7 tusipoendelea na ujenzi wa reli hii tukakamilisha, fedha hizi tulizozilaza pale chini zitakuwa hazina maana. Kwa hiyo, kwa njia yoyote kwa vyovyote, tutakopa, tutaangalia njia rahisi, sijui zitakazotufaa za kukopa kwa sababu fedha hizi hatutazitoa kwenye tozo wala hatutazitoa kwenye kodi tunazozikusanya ndani ili kukamilisha.

"Ni lazima tutakopa ili kukamilisha mradi huu, ni lazima tumalize na nitoe maelekezo kwamba tunapokwenda kumaliza kipaumbele kitolewe kwa yale matawi ambayo yanatuunganisha na nchi za jirani ili tuweze kurahisisha biashara zetu.

"Tuweze kuingia kwenye masoko ya nchi jirani, itapendeza tukimaliza reli humu ndani Tanzania, lakini ni vizuri zaidi twende kwenye nchi jirani tuunganishe huko ili fedha hii tunayoikopa na kujenga reli hii ifanye kazi, izalishe na turudishe," alisema.

Rais Samia alionya kuwa uzembe katika utekelezaji wa mradi huo utakuwa na manufaa kwa nchi zingine zitakazotumia fursa hiyo na kuiacha nyuma Tanzania.

"Mimi niko pamoja nanyi, tutaangalia mikopo inayotufaa, tukiongozwa na Gavana wa Benki Kuu (BoT) na waziri yupo hapa, tutachukua tumalize reli kama tulivyopanga ili ifanye kazi, itengeneze fedha tuweze kulipa mikopo tunayoichukua," alisema.

Aliongeza kuwa mpango uliopo ni wa kujenga vipande vya reli kutoka Uvinza hadi Msongati, Burundi na kuendelea hadi Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) pamoja na Isaka hadi Kigali, Rwanda.

### UNUNUZI MABEHEWA

Rais Samia pia alisema serikali tayari imeingia mikataba ya ununuzi wa mabehewa ya abiria 89, vichwa vya treni ya umeme 19, seti za treni za kisasa 10 zenye mabehewa 80 na mambo yote hayo yanagharimu dola za Marekani 381,428,465.

Pia alisema serikali inakamilisha ununuzi wa mabehewa ya mizigo 1,430 yenye thamani ya dola za Marekani 127, 206,300.

Alionya kuwa hatamfumbia macho mtu yeyote atakeyechezea pesa za miradi hiyo ya serikali na hata kama mtu huyo atakuwa ameondoka madarakani, atamchukulia hatua dhidi yake.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli (TRC), Masanja Kadogosa, alisema mkataba uliotiwa saini jana utafanya jumla ya uwekezaji wa serikali kufikia Sh. trilioni 14.73, thamani ya mkataba wa jana ni Sh. trilioni 4.406 na muda wa ujenzi utakuwa miezi 46.

# Wadau wa haki wataka tume uchunguzi kuhojiwa Mwingira

**Na Waandishi Wetu**

SIKU moja baada ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, kuliagiza Jeshi la Polisi kumhoji Kiongozi wa Kanisa la Efatha, Nabii Josephat Mwingira, wadau wa haki na wanasiasa wamedai kilichotamkwa na kiongozi huyo wa kiroho ni uhalisia wa mengi waliyopitia baadhi ya watu.

Baadhi ya wadau hao pia wamependekeza kuundwe Tume ya Uchunguzi itakayoongozwa na Jaji mstaafu wa Mahakama ya Rufani itakayochunguza na kubainisha madhila waliyopitia watu mbalimbali ikiwamo kuporwa mali zao, kudhalilishwa, kufunguliwa kesi na kutekwa.

Wamesema kuwa badala ya nabii huyo kuhojiwa, iko haja Rais kuweka utaratibu maalumu wa watu kueleza waliyopitia na kwamba kufanya hivyo, kutasaidia walichokiita 'kuliponya taifa'.

Juzi Waziri Simbachawene aliliagiza Jeshi la Polisi kumhoji Nabii Mwingira kutokana na matamshi yake ya hivi karibuni kwamba alinusurika kifo dhidi ya maofisa wa serikali na kuteketezwa kwa mali zake za mabilioni.

Muda mfupi baada ya agizo hilo, Jeshi la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, liliagiza ndani ya saa 24 kuanza kuhojiwa kwa Nabii Mwingira juu ya tuhuma mbalimbali alizozitoa dhidi ya serikali, ikiwamo njama za maofisa wa serikali kutaka kumuua.

Katika ukurasa wake wa Twitter, Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, aliandika: "Kilichosemwa na Askofu Mwingira kiliwatokea watu wengi nchini katika miaka mitano iliyopita...watu walifukuzwa kazi na wengine kuporwa mali zao. Jawabu ni kuunda Tume ya Uchunguzi itakayoongozwa na jaji mstaafu wa Mahakama ya Rufani.

"Ni muhimu kuunda tume ya majaji itakayoongozwa na jaji mstaafu wa Mahakama ya Rufani kuchunguza matukio yote ya... (alitaja matukio), watu kupotea. Watu kubambikiwa kesi na kulipa fidia na kufutiwa rekodi za jinai kwa watu wote watakaobainishwa na tume.

"ACT-Wazalendo iliweka hili kwenye ilani yake ya uchaguzi ya mwaka 2020. Watu waliteswa sana, waliumizwa sana. Tume ya Uchunguzi kuchunguza malalamiko kama ya Askofu Mwingira, wengi hawajasema madhila yaliyowakuta..."

Aliyekuwa Mbunge wa Iringa Mjini, Mch. Peter Msingwa, aliandika: "Rais Samia Suluhu Hassan nashauri uweke utaratibu maalumu kwa watu waliofanyiwa vitendo vya ukiukaji wa haki zao kupigwa, kuteswa, kutishwa na wengine kunyang'anywa mali zao ili watoe malalamiko yao. Hii itasaidia sana kuliponya taifa..." Wakili Jebra Kambole aliandika: "Bila tume huru ya kuchunguza madhila waliyokutana nayo watu, badala ya kuliponya taifa tutazidi kuligawa taifa! Maana wengi sana walilia machozi na kupoteza ndugu zao, sasa kusahau au kusamehe hilo siyo rahisi, tujifunze kutoka kwa wengine."

Mwanachama wa CHADEMA, Liberatus Mwang'ombe, aliandika "Tumtie moyo na kumhakikishia amani kila mtu anayeeleza madhila yaliyotokea. Tunahitaji kuwatia moyo ili wengi zaidi watoke hadharani kuelezea waliyopitia. Tusiweke mazingira ya kuwatia hofu na kuwa 'bully' (myanyanyaso mtandaoni) badala yake tuwalinde na kuwatia moyo."

Wiki iliyopita, Zitto aliandika kupitia ukurasa wake wa Twitter madhila aliyopitia ikiwamo madai ya kuchomwa moto kwa shamba lake la korosho na nyumba yake, huku akieleza maumivu makali aliyokuwa nayo kutokana na jambo hilo na hadi leo hakuna aliyekamatwa.

### UCHUNGUZI WAENDELEA

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limesema linaendelea na uchunguzi wa kauli alizozitoa Nabii Mwingira kuhusu tuhuma mbalimbali alizozitoa dhidi ya serikali ikiwamo njama ya maofisa wa serikali kutaka kumuua.

Mwanzoni mwa wiki hii, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, aliagiza Jeshi la Polisi Kanda Maalum kumhoji Mwingira kutokana na matamshi yake.

Kutokana na kauli hiyo, jeshi hilo liliagiza ndani ya saa 24 kuanza kuhojiwa kwa kiongozi huyo wa kiroho kuhusu tuhuma mbalimbali alizozitoa dhidi ya serikali.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kamanda wa Kanda hiyo, Jumanne Muliro, alisema uchunguzi unaendelea na taarifa zaidi zitatolewa baada ya kazi hiyo kukamilika.

"Jeshi la Polisi limefikia hatua hiyo baada ya kufuatilia kwa umakini kauli zinazodaiwa kutolewa na Mwingira na kuona kama zinajenga hofu na chuki kwa wananchi dhidi ya serikali yao," alisema Muliro.

HABARI KITAIFA

## Uamuzi kesi ndogo ya kina Sabaya leo

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha leo inatarajia kutoa uamuzi wa ama kukataa au kumruhusu shahidi wa 13 wa Jamhuri, Ramadhani Juma (39) kutoa ufafanuzi kuhusu video za CCTV zinazowaonyesha vijana wanaodaiwa wa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, wakiingia Benki ya CRDB na kukabidhiwa Sh. milioni 90.

Mahakama hiyo itatoa uamuzi huo katika kesi ya uhujumu uchumi namba 27 inayomkabili Sabaya na wenzake sita mahakamani huko.

Katika shauri hilo, mbali na Sabaya washtakiwa wengine ni Sylvester Nyengu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).Desemba 17, mwaka huu, mawakili wa upande wa utetezi, wakiongozwa na Sylvester Kahunduka, walipinga mahakamani huko shahidi huyo, kuzielezea video hizo wakidai hakuhusika kuziandaa.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Felix Kwetukia, alidai kwamba shahidi huyo, ni mhusika katika kuielezea video hiyo kwa kuwa ndio mpelelezi mkuu wa kesi hiyo.

"Mheshimiwa hakimu, shahidi wetu ndiye mpelelezi mkuu katika kesi hii, na alitumia taarifa fiche kuwatambua washtakiwa hawa, pia alitumia video hizi kuchunguza tuhuma zinazowakabili washtakiwa katika shauri ili kuthibitisha kama ni za kweli," alidai.

Shahidi alidai mahakamani huko kwamba video za CCTV zilikuwa zikionyesha matukio ya vijana wanaodaiwa ni wa Sabaya wakiingia na kutoka Benki ya CRDB Tawi la kwa Murombo jijini Arushwa baada ya kupewa rushwa ya Sh. milioni 90 na mfanyabiashara Francis Mroso.

Ramadhani ambaye ni Ofisa Uchunguzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Arusha, aliwasilisha taarifa mahakamani iliyodaiwa kuwa na mchanganuo wa mgawanyo wa Sh. milioni 90 zinazodaiwa kuchukuliwa kwa mfanyabiashara Mroso.

Alidai kuwa baada ya kupata fedha hizo, wakiwa katika hoteli ya Tulia Lodge, walikunywa na kula vyakula na Sabaya anadaiwa alitoa mgawo kwa vijana wake kutokana na kazi waliyofanya.

"Baada ya kazi mgawo ulikuwa hivi: John Odemba Sh. 300,000; Sadick Kiiza Sh. 400,000; Nathan Msuya Sh. 500,000; Watson Sh. 600,000; Enock Togolani Sh. milioni 1.5; Sylvester Nyegu Sh. milioni 2.2; na Jackson Macha Sh. milioni 1.4," alidai.

Katika kesi hiyo, shtaka la kwanza ni la kuongoza genge la uhalifu kinyume cha sheria linalowakabili washtakiwa wote; shtaka la pili ni la kujihusisha na vitendo vya rushwa na linalomkabili mshtakiwa wa kwanza (Sabaya) peke yake; na shtaka la tatu ni la kujihusisha na vitendo vya rushwa, linalomkabili mshtakiwa wa kwanza peke yake.

Shtaka la nne ni la matumizi mabaya ya madaraka, linalomkabili Sabaya peke yake na shtaka la tano ni la utakatishaji wa fedha na linalowakabili washtakiwa wote saba.

# Waganga tiba asili mabalozi wa uhamasishaji chanjo UVIKO-19

**Na Mary Geofrey,**
MANYONI

WAGANGA 28 wa tiba asili, Kata ya Ipande Halmashauri ya Itigi, wilayani Manyoni, mkoani Singida, wamechanja chanjo ya UVIKO-19 na kukubali kuwa mabalozi wa kuhamasisha wagonjwa wao ambao hawajapata chanjo hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana wilayani hapo, Katibu wa Waganga wa Tiba Asili katika kata hiyo, Nyanza Ndambuli, alisema wameamua kuchanja na kutoa elimu kwa wateja wao baada ya wao kuelimika kuhusu chanjo ya UVIKO-19.

Aliahidi kuwa mabalozi wazuri kwa wateja wao ambao wanatoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya kijiji na kata hiyo.

"Nimechoma chanjo ya UVIKO-19, kwa pamoja kama waganga wa tiba asili tumekubaliana kutoa elimu kwa wateja wetu pia. Kwa siku napokea wateja kuanzia wanne ina maana akija mteja mwenye corona ni rahisi kuniambukiza na kuambukiza wengine, lakini tukichanja tunakuwa salama wote," alisema Ndambuli.

Naye Mtafiti wa Tiba Asili, Hussein Rajabu, alisema walipatiwa elimu ya chanjo na walikubali kuchanja na wapo tayari kuhamasisha waganga wengine wapate chanjo hiyo.

"Tulikutana waganga 28 na wote kwa umoja wetu tulikubali kupata chanjo ya UVIKO-19. Tumekubaliana kuanza kuzungumza na wateja wetu kwanza wakapate chanjo ndiyo tuwapatie matibabu ili kuepuka kuenea kwa ugonjwa huu," alisema.

Naye Katibu wa Waganga wa Tiba asili, Halmashauri ya Itigi, Halima Mbalamwezi, aliishukuru serikali kwa kutambua umuhimu wa waganga wa kienyeji na kuamua kuwapatia elimu ya chanjo na kuwachanja.

"Kwa kutambua umuhimu wetu, nasi tumeamua kuwa mabalozi kwa wateja wetu, lakini na waganga wenzetu ambao hawajapata chanjo ili tuendelee kutoa huduma tukiwa salama na wateja wetu nao wawe salama," alisema.

Kwa upande wake, Diwani wa Kata ya Ipande, Kedmon Mpondo, alisema kwa kushirikiana na Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Itingi, Emmanuel Mallange, walifanya kikao na waganga hao ili kuwapa elimu na chanjo hiyo.

Diwani huyo ambaye ni mwenyekiti wa huduma za afya, katika halmashauri hiyo, aliahidi kuendelea na kazi ya kuwafikia waganga wengine waliobaki katika kata yake.

"Tunaamini kuwa kuwafikia waganga hawa, nao watawafikisha taarifa kwa wenzao na wateja wanaokwenda kuwapatia matibabu katika maeneo yao," alisema Mpondo.

Naye Mganga Mkuu wa Mkoa wa Itigi, Victorina Ludovick, aliwapongeza wataalamu wa afya ngazi ya halmashauri kwa kushirikiana na diwani kulifikia kundi hilo muhimu.Alizitaka halmashauri nyingine kuiga mfano huo, utakaosaidia kufikia watu wengi na kuuvusha mkoa huo kutoka nafasi ya mwisho kitaifa kwa utoaji wa chanjo ya UVIKO-19.

Hatua hiyo ni mwendelezo wa ziara ya Wataalamu wa Afya, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), katika Kampeni ya Kuhamisha na Utoaji wa chanjo ya UVIKO-19, katika Mpango Shirikishi na Harakishi Awamu ya Pili.

Kampeni hiyo inayolenga kufikia wananchi nyumbani, mtaani, shambani na sehemu za biashara, inatekelezwa na wizara hiyo kupitia Kitengo cha Elimu kwa Umma kwa lengo la kufikia asilimia 60 ya Watanzania.



Diwani wa Kata ya Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Salome Mnyawi, akiweka shada la maua kwenye kaburi la mfanyabiashara wa madini ya Tanzanite, Ruth Mmassy, anayedaiwa kuuawa na mtoto wake jijini Arusha juzi. PICHA: GIFT THADEY

# TMA yahadharisha mvua kubwa Dar, Pwani

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imetoa tahadhari kuwa mvua itaendelea kunyesha katika maeneo ya mikoa ya Pwani, Dar es Salaam na Kanda ya Ziwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Mtaalamu wa Hali ya Hewa kutoka TMA, Joyce Makwata, alisema kwa mikoa ya Kanda ya Ziwa (Mwanza, Mara, Kagera na Geita) mvua zinazoendelea ziko nje ya msimu na zinatarajiwa kuendelea mpaka katikati ya mwezi ujao.

"Mikoa mingine hizi ni mvua za msimu ukiondoa mikoa ya Kanda ya Ziwa ambayo mvua zake mara nyingi zinaisha Desemba, lakini hizi zitaenda mpaka Januari bado zitakuwa zinanyesha, hivyo tunawashauri wananchi kuendelea kuchukua tahadhari ya madhara yanayoweza kutokea," alisema Makwata.

Pia alisema wananchi waendelee kufuatilia taarifa rasmi zinazotolewa na TMA ili kuchukua tahadhari.

Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omari Kumbilamoto, akizungumza na Nipashe jana, alisema mpaka sasa bado hakuna madhara makubwa yaliyotokana na mvua katika jiji hilo.

"Athari kubwa ambazo ziko mpaka sasa ni baadhi ya maeneo kuzungukwa na maji, lakini athari kubwa zaidi ya hapo hazijaripotiwa," alisema Kumbilamoto.

Pia alisema kwa sasa wananchi wanatakiwa kuendelea kuchukua tahadhari na kufuata maelekezo na ushauri unaotolewa na mamlaka husika.

"Lakini hiki ndicho kipindi cha kuimarisha miundombinu. Kwa mfano kwa sasa tunakazania na kusubiri kuona kama tutakamilisha ujenzi wa kingo za Mto Msimbazi ili kukabiliana na athari za mvua kwenye Mto Msimbazi," alisema.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera, Prof. Faustine Kamuzora, alisema mvua zinazoendelea kunyesha mkoani humo bado hazisababisha madhara, lakini zimeleta faida kwenye kilimo.

"Sisi tumepata mvua za wastani na bado zinaendelea. Zimefanya mazao kustawi kwa sababu tuliwashauri wananchi kulima mazao ya muda mfupi, hatujapata madhara makubwa tunashukuru Mungu," alisema.

Mvua zinazoendelea sasa kwenye baadhi ya mikoa nchini zilitabiriwa na TMA Septemba, mwaka huu, kwa mikoa inayopata mvua za msimu baadhi zilitarajiwa kumalizika mwezi huu.

RIPOTI MAALUM

# Shughuli za binadamu zinavyoharibu barabara

- Wananchi wajitetea kinachowasukuma
- TARURA, TANROADS waanika hasara

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, akitoa elimu kwa wakazi wa Chamaguha, Manispaa ya Shinyanga kuhusu athari za shughuli za kibinadamu kando ya barabara hivi karibuni. PICHA: ZOTE MARCO MADUHU

NI majira ya saa 12 asubuhi, jua likiashiria mawio, kwa mbali anaonekana mama aliyejifunga kitenge cheusi na madoa ya kijana, akilima pembezoni mwa daraja la Iwelyangula wilayani Shinyanga, barabara kuu ya Shinyanga - Dar es Salaam.

Anastazia Simon, mkazi wa Kitangili jirani na daraja hilo la Iwelyangula, katika udadisi wa Nipashe, anakiri kwamba yeye na wananchi wenzake wamekuwa wakilima kando ya barabara hiyo jirani na madaraja ili kuwa na uhakika wa kupata maji ya kutosha kwa ajili ya shughuli zao za kilimo.

Mama huyo ambaye kimwonekana ana umri wa makamo, ana ufafanuzi zaidi, akitamka:

"Kinachotusukuma kulima kando ya barabara hii hasa karibu na madaraja ni urahisi wa kupata maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

"Mtaa wetu huu wa Iwelyangula hauna bwawa la maji, tunategemea maji kwenye mto huu unaopita kwenye daraja hili.

"Maji yakikauka mtoni, watu wanachimba mashimo ndani ya mto chini ya hili daraja, wanapata maji ya kumwagilia mazao yao.

"Kama serikali inaona kuna madhara sisi kuendesha shughuli zetu za kilimo karibu na madaraja, ituchimbie bwawa la maji ili tusiharibu miundombinu ya barabara."

Mkazi mwingine wa mtaa huo, John Masanja, anaunga mkono utetezi wa jirani yake huyo huku akiutaja uchimbaji wa mchanga kuwa kiini kingine cha uharibifu wa barabara mkoani Shinyanga.

Anasema kuwa katika kujitafutia riziki, baadhi ya vijana wamekuwa wakivamia hifadhi za barabara na kuchimba michanga, hasa chini ya madaraja.

"Unakuta watu wanachimba mchanga ndani ya mto, wengine wanasogea hadi kwenye daraja, wanapochimba kwenye daraja panakuwa na shimo kubwa, mvua ikinyesha daraja linasombwa na maji kwa kuwa halina uwezo wa kuhimili maji," anasema Masanja.

Paul James, mkazi mwingine wa eneo hilo, anapaza sauti kwa serikali kwamba inapaswa kutoa elimu kwa wananchi juu ya uhifadhi wa barabara ili waache kufanya shughuli za kibinadamu pembezoni mwa barabara.

Anasema hata kuharibika kwa daraja hilo la Iwelyangula kumetokana na wananchi kuchimba mchanga chini yake pamoja na shughuli za kilimo zinazoendelea karibu na daraja hilo.

### KAULI YA MWENYEKITI

Mwenyekiti wa Mtaa wa Iwelyangula, Robert Mnyeleshi, anasema wananchi hawajapatiwa elimu ya madhara ya kulima pembezoni mwa barabara, hivyo wanatenda makosa pasi na kujua kwamba wanakiuka sheria na miongozo ya kiserikali.

"Mimi mwenyewe sina hiyo elimu ya kutolima kando ya barabara. Sasa nitawezaje kuelimisha wananchi kitu nisichokifahamu?" Alihoji.

Hata hivyo, mwenyekiti huyo alisema wanakusudia kuitisha mkutano wa hadhara na kuwaalika wataalamu kutoka Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kuhifadhi barabara.

### AGIZO LA DC

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, ukaguzi wake wa ujenzi wa daraja la Iwelyangula linalounganisha kata za Kitangili na Chamaguha, Manispaa ya Shinyanga, anakemea tabia ya baadhi ya wananchi kufanya shughuli za kilimo pembezoni mwa barabara, akionya kuwa zinaharibu miundombinu hiyo.

Daraja hilo linajengwa upya baada ya kusombwa na maji wakati wa msimu uliopita wa mvua.

Mboneko anawataka wananchi wilayani Shinyanga kutolima mazao ndani ya hifadhi ya barabara kwa kuwa miundombinu hiyo inapoharibika, serikali inaingia gharama kubwa za matengenezo.

"Fedha zinazotumika kukarabati madaraja, serikali ilipaswa kuzielekeza kwenye miradi mingine muhimu.

"Ni marufuku wananchi kulima kando ya barabara, kalimeni huko kwenye mashamba ambayo si hifadhi ya barabara.



Mwonekano wa Daraja la Iwelyangula linalounganisha kata za Chamaguha na Kitangili, Manispaa ya Shinyanga, likiwa limebomoka kutokana na shughuli za kibinadamu kwenye daraja hilo.

Ninawaagiza viongozi wa maeneo haya, wananchi ambao wamelima kandokando mwa barabara wavune mazao yao na wasiliane tena.

"Juni mwaka huu nilifika kwenye daraja hili la Iwelyangula ambalo linaunganisha kata mbili za Chamaguha na Kitangili na kukuta limebomoka kwa kusombwa na maji.

"Kiini cha tatizo ni wananchi kufanya shughuli za kibinadamu kwenye daraja. Serikali tumeingia gharama ya Sh. milioni 428 kulijenga tena daraja hili, fedha ambazo tungezielekeza kwenye miradi mingine," anasema.

### DARASA LA TARURA

Meneja wa TARURA, Manispaa ya Shinyanga, Salvatory Yambi, anasema barabara nyingi, hasa kwenye madaraja na makaravati, zimekuwa zikiharibiwa na shughuli za kibinadamu.

Kaimu Mratibu wa (TARURA) mkoani Shinyanga, Respicius Matungwa, anasema elimu ya uhifadhi wa barabara bado haijatolewa kwa wananchi wengi.

Kwa kutambua hilo, Matungwa anawataka watendaji wa vijiji, mitaa na vitongoji watoe elimu kwa wananchi kuhusu uhifadhi wa barabara.

"Wananchi wanapofanya shughuli zao za kibinadamu kwenye hifadhi za barabara, wanaziba mitaro na kuathiri uso wa barabara na hivyo kusombwa na maji. Unakuta kifusi kipo juu ya barabara kimesukumwa na maji," anasema.

Mratibu huyo ana angalizo la kisheria, akisema hifadhi ya barabara ni eneo ambalo limetengwa kupitia sheria namba 13 ya mwaka 2007, inayozungumzia utunzaji wa miundombinu ya barabara.

Anazitaja aina za barabara na eneo la hifadhi ya barabara ambalo mwananchi hapaswi kuliendeleza kwa mujibu wa sheria.

"Kwa barabara kuu, mfano barabara ya kutoka Arusha-Mwanza, Dar-Mwanza, Dar-Bukoba, hizo unatakiwa kuacha mita 60 kutoka katikati ya barabara, yaani kushoto mita 30 na kulia mita 30.

"Barabara za mkoa unaacha mita 30 kutoka katikati ya barabara. Kwa barabara za wilaya unatakiwa kuachwa mita 40 kutoka katikati ya barabara na barabara za vijiji ni mita 30 kutoka katikati ya barabara.

"Kwa upande wa barabara za mitaa ni mita 25 kutoka katikati ya barabara. Hiyo ndiyo hifadhi ya barabara," anafafanua.

Matungwa anawataka wananchi kutofanya shughuli za binadamu karibu na barabara kwa kuwa ni kinyume cha sheria na kunasababisha hasara kubwa kwa serikali.

Kwa mujibu wa TARURA mkoani Shinyanga, katika bajeti yao ya matengenezo ya barabara za mkoa huo kwa mwaka wa fedha 2020/21, walitenga Sh. bilioni 7.6.

Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) mkoani Shinyanga, Mibara Ndirimbi, anasema kutokana na uharibifu wa barabara mkoani humo, kwa mwaka wa fedha 2020/21 walitenga Sh. bilioni 13.4 kwa ajili ya matengenezo ya barabara, madaraja na makalavati.

# RC ampa kibarua DC kero ya bajaji

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, amemwagiza Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, kuwakutanisha madereva wa bajaji ndani ya wiki moja kupitia umoja wao na wataalamu wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa ili kutazama kero zinazowakabili na kuzifanyia kazi .

Sendiga alitoa agizo hilo jana katika ukumbi wa CCM Mkoa wa Iringa wakati wa kikao cha pamoja cha madereva hao wa bajaji.

Alisema ya sikukuu ya Mwaka Mpya afanye jitihada za kukutanisha viongozi wa manispaa na vijana hao ili kupunguza malalamiko yao ya mara kwa mara.

"Kupitia vikao ndipo tunapata majibu ya changamoto zinazowakabili madereva wa bajaji na kuzifanyia kazi. Nikutake Mkuu wa Wilaya fanya hima kuandaa kikao cha pamoja kati ya ofisi ya manispaa na bajaji ili kujua kero hizo na kuzitatua," alisema.

Pia alisema suala la kuwapo kwa zuio la kusajili bajaji mpya katika Manispaa ya Iringa analitambua na anaendelea kulifanyia kazi ili bajaji hizo ziruhusiwe kusajiliwa na kuendelea na kazi kama kawaida.

Katika hatua nyingine, Sendiga aliwataka madereva wa bajaji kuhakikisha wanatimiza wajibu wao kwa kufuata sheria za usalama barabarani. Alisema suala la kufukuzwa na polisi halitakuwapo iwapo watafanya kazi kwa kufuata sheria.

Alisema madereva hao wa bajaji baadhi yao wamekuwa wakifanya kwa makusudi kuvunja sheria na pindi wanapofuatwa ili kuwajibishwa, wamekuwa wakiwakimbia polisi jambo ambalo si zuri kwao kwa ajili ya usalama.

Mwenyekiti wa Umoja wa Madereva wa Bajaji Iringa, Melabu Kihwele, alisema baadhi ya askari polisi wamekuwa wakinyanyasa na pale wanaposimama kuzungumzia kero hizo, wamekuwa wakionekana kama ni wahuni jambo ambalo si sahihi.

Kihwele alisema kuna zaidi ya vijana 50 wamefika ofisini kwake kulalamika kuwa kuna vibao vimewekwa katika barabara wanayopita kutokea Neema Craft, kuzuia bajaji kupita kwa sababu ni sehemu ya kuvuka watu wenye ulemavu jambo ambalo hakushirikishwa.

Pia alitaja kero nyingine kuwa ni kutokuwa na leseni kwa madereva wa bajaji wengi mkoani Iringa na hadi sasa zaidi ya madereva 180 hawana.

# Kamanda Sirro asema uhalifu umepungua

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Jeshi la Polisi, IGP Simon Sirro, amesema uhalifu nchini kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita hadi sasa umepungua kwa kiasi kikubwa, hasa unyang'anyi wa kutumia silaha.

Vilevile, amesema matukio ya ajali na makosa ya usalama barabarani kwa ujumla yamepungua kwa asilimia 14.

Akihojiwa usiku wa kuamkia jana kwenye kipindi cha Dakika 45 kinachorushwa na ITV, alisema makosa ya jinai kwa mwaka jana na mwaka huu yamepungua kwa asilimia 3.5 na makosa ya usalama barabara yamepungua kwa asilimia 14.

Alisema mafanikio hayo ni kutokana na ushirikinao baina ya Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya ulinzi na usalama pamoja na wananchi, akibainisha kuwa Mkoa wa Kipolisi wa Kibiti uliokuwa na matukio ya mauaji ya viongozi na askari polisi, sasa hauna uhalifu wa aina hiyo.

"Hii haina maana kwamba sisi ni kisiwa cha amani, bado tuna kazi ya kufanya kwa sababu amani ni lazima tuendelee kuisimamia kwa pamoja, ukilegea tu wahalifu wanachukua nafasi na kufanya uhalifu ambao mwisho utakuwa ni tishio kwetu.

"Miaka ya nyuma hata ukienda benki ukichukua Sh. 40,000 unakuwa na shaka ukienda barabarani itakuwaje, lakini kwa sasa tunakwenda vizuri na niwapongeze raia wote wema, kuna wengine wanatuchukia kwa sababu ya matendo yao mabaya ila mimi kazi yangu ni kusimamia sheria," alisema.

IGP Sirro alionya kuwa askari polisi watakaoonekana kukiuka sheria kwa kujihusisha na makosa ya uhalifu, wananchi watoe taarifa katika ofisi zao za malalamiko, mkuu wa wilaya au katibu tarafa ili wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria.

Pia alikemea wizi unaofanywa na baadhi ya watu, hasa wa televisheni na pikipiki, akizitaka kamati za ulinzi na usalama kutimiza majukumu kikamilifu.

Kuhusu ulinzi shirikishi, IGP Sirro alikumbusha kuwa halmashauri zinapaswa kutunga sheria ndogo na kila Mtanzania ana wajibu moja kwa moja ikiwamo kuchangia vijana wanaofanya ulinzi shirikishi ili usalama uendelee kuimarika.

"Niwaombe sana Watanzania kwamba usikubali kwenda kulala kwenye nyumba yako bila kuhakikisha kwamba umeacha mlinzi kwenye mtaa, pia wale ambao wamebahatika kupata mageti, maghorofa wawasaidie wale vijana wanaolinda kwenye mtaa.

"Ukisema mimi nina mlinzi huyo hasaidii sana kwani akishabananishwa watakufuata kwenye ghorofa lako, lakini wakija wakikuta mko watu wengi barabarani hata wao ni binadamu, wanaogopa na hawawezi kuleta matatizo, nisisitize kwenye vijiji vyote kuwa na vikundi vya ulinzi shirikishi," alisema.

IGP Sirro pia alisema wanaendelea na mapambano dhidi ya rushwa, akitaja kuwa kuna askari wamefukuzwa kazi kutokana na kujihusisha na vitendo hivyo.

Kwa mujibu wa IGP Sirro, baadhi ya askari wanashawishiwa kupokea rushwa, pia wakati mwingine polisi kushawishi, hivyo ni muhimu Watanzania wanaoshawishiwa, kutoa taarifa ili hatua za kisheria zichukuliwe.

"Tunajua rushwa ni adui wa haki na hasa kwa upande wa Jeshi la Polisi tunaosimamia haki. Kukishakuwa na rushwa, uhalifu, ujambazi, ajali zitazidi. Kwa hiyo, kwetu suala hilo ni kosa kubwa, niwaombe Watanzania wakiona kuna askari anakengeuka, watoe taarifa, pia nanyi msishawishi polisi kupokea rushwa," alionya.

Alipotakiwa kutoa ufafanuzi kuhusu kinachoitwa 'taarifa za kiintelijensia' ambazo wakati mwingine zimekuwa zikitumika kuzuia vyama vya siasa kufanya mikutano nchini, IGP Sirro alisema:

"Ukitaka kujua maana ya intelijensia utamaliza miaka mitano kukuelezea uweze kuelewa. Ukizungumzia taarifa za intelijensia, ina vitu vingi sana na sina sababu za kueleza hapa, hivi unajua kuna vitu naweza kukwambia (mtangazaji) na vingine nisikwambie?"



Wafanyakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakichimba makaburi katika eneo la Kitunda Mwanagati kwa ajili ya kuzika miili inayohamishwa kutoka Vingunguti jana. PICHA: JUMANNE JUMA

# Uuzaji moja kwa moja watajwa suluhu uchumi katika UVIKO-19

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI sekta karibu zote za uchumi duniani zimepata hasara kubwa kutokana na janga la UVIKO-19, uuzaji wa moja kwa moja umeendelea kuwa thabiti na hata kukua katika kipindi hiki cha baa la ugonjwa huo. "Uuzaji wa moja kwa moja ni njia ya mauzo inayotumiwa na kampuni kusambaza bidhaa zao moja kwa moja kwa watumiaji pasi na kufungua maduka na kuajiri wauzaji kama ilivyo ada," alisema Mratibu wa Kanda ya Afrika Mashariki wa Qnet, Muqtadir Suwani, juzi.

Akizungumza na waandishi wa habari, mratibu huyo alirejea ripoti ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) inayoonyesha kuwa uchumi wa dunia ulipungua kwa asilimia 4.4 mwaka 2020.

"Lakini wakati huo huo, ripoti ya hivi karibuni ya uuzaji wa moja kwa moja, iliyochapishwa na Shirikisho la Dunia la Mashirika ya Uuzaji wa Moja kwa Moja (WFDSA), inaonyesha mauzo ya moja kwa moja duniani yameongezeka kwa asilimia 2.3 kutoka dola bilioni 175.3 mwaka 2019 hadi dola bilioni 179.3 mwaka 2020," alisema.

Akifafanua zaidi, Suwani alisema IMF hivi karibuni ilipandisha makadirio yake ya ukuaji wa uchumi mwaka 2021 hadi asilimia sita kutoka asilimia 5.5, na miradi ya ukuaji wa asilimia 4.4 katika 2022.

"Sambamba na makadirio haya, kampuni ya mauzo ya moja kwa moja ya Qnet, ilipata ukuaji wa hadi asilimia 65 katika baadhi ya masoko ya Afrika," alibainisha.

Akielezea chanzo cha mafanikio ya kampuni hiyo, alisema ongezeko la mahitaji ya ununuzi wa mtandaoni umewezesha kampuni za uuzaji wa moja kwa moja kukua kwa kasi hasa katika kipindi cha janga la corona.

"Kutokana na ongezeko la matumizi ya intaneti na malipo kupitia simu za mkononi na mtandaoni, soko la kimataifa la bidhaa na huduma za kidijitali linapanuka kwa viwango ambavyo havijawahi kushuhudiwa," alisema. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Trade Mark East Africa (TMEA) 2020, asilimia 91 ya waliohojiwa Uganda walisema kuwa wamefanya ununuzi wa mtandaoni mwaka 2020, na Kenya walikuwa asilimia 86 wakati Tanzania walikuwa asilimia 81.3, Burundi ni asilimia 58.8 na Rwanda ni asilimia 50.

Afrika inakadiriwa kuwa eneo jipya la ukuaji wa soko la uuzaji wa moja kwa moja. Uchambuzi wa Uchumi wa Benki ya Dunia unaripoti kuwa nchi za Kiafrika zimejikwamua haraka kutoka kwa janga la UVIKO-19 kupitia matumizi ya kidijitali na mfumo wa biashara ya mauzo ya moja kwa moja.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ushirikiano polisi, wananchi uendelee kudhibiti uhalifu

**JANA** Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro, alisema matukio ya uhalifu yamepungua kwa asilimia 3.5, huku akiwataka wananchi kuwajibika kulinda nyumba na mali zao wakati huu wa sikukuu.

Alisema mafanikio hayo ni kutokana na ushirikiano baina ya wananchi na vyombo vingine vya ulinzi na usalama nchini.

Hii ni habari njema kwa kuwa ushirikiano huo umezaa matunda na unatukumbusha enzi za polisi jamii kipindi ambacho ushirikiano ulikuwa mkubwa na kuwezesha kukabili matukio mengi kiasi cha kukabili uhalifu mkubwa na mdogo.

Hivi karibuni matukio ya uhalifu yaliibuka na kuonekana yameongezeka huku malalamiko mengi yakiwa mtaani kuhusu watu kuvamiwa kwenye nyumba zao kuibiwa vitu mbalimbali.

Wapo waliodai kuibiwa magari, wengine kuibiwa vifaa vya magari, vifaa vya ndani kama TV na mali nyingine, huku kukiwa na matukio ya kuvunja maduka na magodauni, jambo ambalo liliwafanya wengi kupaza sauti na kulitaka Jeshi la Polisi kuchukua hatua.

Kwa mujibu wa IGP Sirro ilifika mahali watu waliogopa kwenda kuchukua hata Sh. 40,000 kwenye ATM, lakini kwa sasa hali ni nzuri watu wanaendelea na shughuli zao kama kawaida.

Tunapongeza ushirikiano huo na kuomba uongezeka zaidi hasa kuimarisha ushirikiano kwenye mitaa mbalimbali, jambo ambalo litasaidia kuwa na usalama muda wote.

Lakini kumekuwa na malalamiko kwa baadhi ya askari kushirikiana na wahalifu au matapeli jambo ambalo limepunguza imani kwa wananchi dhidi ya watendaji hao.

Ni muhimu kuchukua hatua madhubuti kwa wale watakaobainika kujihusisha na uhalifu kwa namna moja au nyingine, kwa kuwa kama kwa sasa tunajivunia kupungua kwa uhalifu basi kasoro zilizoko zirekebishwe.

Haya yanayohesabiwa kama mafanikio yaendelee zaidi ifike mahali wananchi wanaweza kulala bila ulinzi au kwa amani zaidi bila hofu ya kuibiwa.

Ni muhimu sana kuelekeza nguvu kwenye kukabili wizi wa kutumia pikipiki na utapeli mtandaoni ambao unashika kasi kwa sasa.

Wizi wa kupora watu pochi kwenye vituo vya daladala, mitaani ni korofi kwa sasa na wanaofanya hivyo ni kama pikipiki zao wanazitumia kwa matukio hayo, na ikiwa watakamatwa na kuchukuliwa hatua itakuwa fundisho na watu wataacha kufanya matukio hayo, ni ukweli kuwa watu wanatoka kwenye jamii yetu na wanafahamika hivyo kwa ushirikiano huo ni muhimu kuchukua hatua ili kukomesha.

Wizi mwingine ni wa utapeli unafanywa na watu ambao wamesajili laini za simu, jambo linalozua maswali kwamba watu wanawezaje kumiliki laini za simu na kuzitumia bila kukamatwa.

Tunajua laini za simu zinasajiliwa kwa alama za vidole, na wakati inafanyika hivyo ilielezwa kuwa itasaidia kupunguza wizi au utapeli wowote unaweza kufanyika, tunapoona matukio haya yanaendelea maana yake kuna ushirikiano mkubwa baina watu hawa na baadhi ya askari wasiowaaminifu.

Kila siku zinaibuka mbinu mpya za uhalifu hasa kwa kutumia mitandao, ni muhimu kuwa na mbinu mpya kwa Jeshi la Polisi kuwa mbele ya jamii na kwa ushirikiano huo kuendelea kupata taarifa zote muhimu kabla ya matukio hayajafanyika.

Ushirikiano baina ya polisi na wananchi unaashiria imani kwa jeshi hilo upo, na sasa ni wajibu wa jeshi hilo kulinda kwa kufanyia kazi mengi yanayolalamikiwa ikiwamo yale yaliyoelezwa na kuelekezwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Vyama vya siasa vya 'mifukoni' vingeishia 2021

Na Sabato Kasika

**VYAMA** vya siasa vya upinzani, ni miongoni mwa taasisi zinazoendelea kutoa mchango katika siasa na demokrasia , pamoja na mijadala mipana inayogusa maeneo mbalimbali yakiwamo ya kiuchumi, uwajibikaji, utawala bora na haki za binadamu.

Mchango huo pia upo katika asasi za kiraia, uhuru wa kujieleza kwa wananchi, wanasiasa na vyama vyenyewe pamoja na amani ili kuleta maendeleo jambo lililoanza tangu kurejeshwa mfumo wa vyama vingi mwaka 1992.

Ilikuwa ni Julai mwaka 1992 serikali ilipoitangazia dunia kuwa imerejesha mfumo wa siasa za vyama vingi, kisha mwaka 1995 uchaguzi mkuu wa kwanza uliovishirikisha vyama vya upinzani ulifanyika.

Hivyo mwaka ujao, itatimia miaka 30 tangu kurejeshwa kwa mfumo huo nchini huku kukiwa na vyama 19 vyenye usajili wa kudumu, kufuatia vingine kufa vyenyewe na baadhi kufutwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, vikionekana kuwa ni vya mfukoni.

Katika idadi hiyo ya vyama 19 vilivyopo, baadhi yake ni kama havipo kutokana na kwamba huwa havisikiki na badala yake huwa vinaibuka wakati wa uchaguzi tu kisha vinaendelea 'kulala usingizi'.

Hatua hiyo ya kuibuka kwa baadhi ya vyama wakati wa uchaguzi, wakati mwingine haiwezi kuwa na manufaa kwa umma, kwani havitaisaidia kuimarisha serikali katika uendeshaji wa nchi.

Ikumbukwe kuwa, vyama vya upinzani vina manufaa mengi ikiwamo kupanua wigo wa majukwaa ya kidemokrasia na uhuru wa kuchagua kushiriki masuala ya siasa za nchi na pia kusaidia serikali iwajibike.

Vyama hivyo pia ni taasisi za kutengeneza wanasiasa na viongozi mahiri wanaoweza kushika nafasi mbalimbali za uongozi, kushiriki harakati za maendeleo kuanzia ngazi ya kitongoji, kijiji, kata, tarafa, wilaya, mkoa na taifa.

Aidha, ni njia mbadala ya kutoa elimu ya uraia, kuchochea serikali kusukuma maendeleo katika maeneo mbalimbali ya nchi, kuimarisha siasa za ushindani miongoni mwa wananchi, wanasiasa na viongozi.

Kwa majukumu kama hayo, vinapokuwapo vyama ambavyo vinavizia wakati wa uchaguzi tu na kisha vinarudi mafichoni, ninaamini kwamba vinaweza visiwe na mchango wowote kwa maendeleo ya nchi.

Mtindo wa baadhi ya vyama kuwa 'mafichoni' na kuibuka wakati unavifanya vikose kuungwa mkono na wananchi, kwa sababu vitakuwa havijulikani, na wala umma utakuwa haujui sera na katiba za vyama hivyo.

Baadhi ya vyama vimekuwa vikiungwa mkono na wananchi katika uchaguzi, kutokana na kwamba vimeendelea kujipambanua tangu viliposajiliwa, havisubiri kujitokeza hadharani wakati wa uchaguzi tu.

Mwaka 2022 unapoingia, ambao vyama vya upinzani vinatarajia kutimiza miaka 30 tangu mfumo huo urejeshwe nchini, visivyofanya siasa vingetafakari na kuchukua kubadilika au njia nyingine ya kujiimarisha.

Inashangaza kuwapo kwa utitiri wa vyama, lakini idadi ya vile vinavyoshiriki katika uchaguzi ni ndogo vikiwamo vinavyoibuka wakati wa uchaguzi, hali ambayo hutafsiriwa kuwa vinajitosa kwa lengo la kuviharibia vingine.

Ni kweli kwamba, mwanzo wa mfumo wa vyama vingi ulikuwa mgumu, kwa vile mfumo wa chama kimoja haukuweza kufutika kirahisi kwani chama tawala hakikujitayarisha kisaikolojia kabla mfumo huo haujaanza kutumika.

Lakini pamoja na hayo, vyama vya upinzani kwa ujumla wake bado vinaweza kujitanua na kupata wawakilishi katika vyombo mbalimbali vya maamuzi kama bunge badala ya kuwa wasindikizaji.

Ili chama chochote cha siasa kionekane kwamba kina uhai, ni vyema kishiriki katika shughuli muhimu za kisiasa na kijamii, lakini kikiwa mafichoni na kusubiri uchaguzi, kinaweza kuwa na kazi ya kusindikiza vingine.

Kuelekea mwaka 2022, ingekuwa vyema kama vyama vya upinzani vinavyoibuka wakati wa uchaguzi, vingejipanga upya ili kuendesha siasa kwa ufanisi badala kusubiri huruma ikiwamo ya kuomba ruzuku ili kujiendesha.

Vyama ambavyo vimekuwa vikiomba ruzuku ili viweze kujiendesha, vingejifunza kutoka kwa vingine ambavyo vimejitahdi kufanya siasa hadi vikafanikiwa kupata sifa za kupata ruzuku hiyo.

Sifa mojawapo ya vyama kupata ruzuku ni hadi viwe vimepata angalau asilimia tano ya kura zote halali zilizopigwa katika uchaguzi mkuu na vyama vyenye wabunge au madiwani.

## Kinamama wapewa mtaji wa biashara

**Na Mwandishi Wetu,** UKEREWE

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, amekabidhi mitaji ya biashara, mitungi ya gesi 66, pikipiki na kompyuta moja kwa kinamama wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Wilaya ya Ukerewe kwa lengo la kuwawezesha kujikwamua kiuchumi.

Mary ambaye ni Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mwanza, alikabidhi vitu hivyo jana alipotembelea ofisi za Umoja wa Wanawake Tanzania wilayani hapa.

"Nimekuja na mtaji wa Sh. 100,000 kwa kila mwanamke, fedha hizi sasa zikasaidie kuongeza vipato vyenu kwa kufanya biashara ndogo," alisema.

Kuhusu mitungi ya gesi, Mary alisema lengo ni kuwasaidia kinamama hao kutumia nishati mbadala na kuachana na matumizi ya kuni ambazo ni chanzo cha uharibifu wa mazingira.

"Nimekuja na nishati mbadala ambayo itasaidia kinamama hawa kuondokana na changamoto za kutafuta kuni na kwa wakati huo huo watakuwa wanatunza mazingira," alifafanua.

Naibu Waziri huyo alisema pikipiki aliyoikabidhi itatumika kuongeza kipato cha umoja huo, ili wainuke kiuchumi na kompyuta itatumika katika shughuli za kiofisi za umoja huo.

Katika hatua nyingine, Mary aliahidi kushirikiana na wanawake hao kumaliza ujenzi wa jengo la UWT Ukerewe.

Awali, akizungumzia kuhusu utalii wa utamaduni, naibu waziri huyo alisema serikali inaunga mkono jitihada za Watanzania wanaojihusisha na ngoma za asili na hivyo itahakikisha inainua vipaji vyao.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake Tanzania Wilaya ya Ukerewe, Neema Mgobela, alimshukuru naibu waziri kwa msaada huo.

"UWT Ukerewe tunakushukuru sana kwa upendo uliotuonyesha siku ya leo na umedhihirisha kwamba sana viatu tulivyokuvisha vimekutosha na uendelee kupambana," alisema.

# Wafugaji wasiosajili mifugo kielektroniki kushughulikiwa

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

SERIKALI imesema itawachukulia hatua wafugaji watakaoshindwa kusajili mifugo yao kwa njia ya utambuzi wa hereni za kielekroniki pindi zoezi hilo litakapofungwa Agosti mwakani.

Angalizo hilo lilibainishwa jana na Mkurugenzi Msaidizi Huduma za Ukaguzi na Ustawi wa Wanyama, Dk. Annette Kitambi, wakati wa utoaji mafunzo ya utambuzi wa mifugo kwa kutumia hereni za kielektroniki mkoani Morogoro.

Ofisa huyo alisema kuwa kwa sasa kinachoendelea ni utoaji elimu kwa wataalamu na viongozi kutoka serikali za mitaa ngazi ya mkoa na wilaya pamoja na wafugaji ambao kwa pamoja watahusika katika kutekeleza usajili huo unaotarajiwa kuanza mwezi ujao.

"Sheria zipo lakini kwa sasa hivi tunafanya kwa kuwahamasisha na kuwaelimisha, zoezi hili litaenda mpaka Agosti mwakani tutakuwa tumemaliza kwa hiari ndipo sheria zitaanza kutumika na sheria imeweka wazi kwamba ikibainika haijatambulika utapigwa faini ya Sh. milioni mbili au kwenda jela miezi sita au vyote kwa pamoja," alisema Dk. Kitambi.

Aliwataka wafugaji kutoa takwimu sahihi za mifugo wanayomiliki pindi utambuzi wa mifugo kwa mfumo wa hereni za kielektroniki utakapoanza mwezi ujao.

Ofisa huyo alisema kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya wafugaji ya kutotoa takwimu sahihi za mifugo yao kwa kuhofia kupunguziwa kutokana na wingi wao, jambo ambalo limekuwa likikwamisha jitihada za serikali hasa katika ugawaji wa maeneo ya malisho.

"Serikali inapoleta sensa ya mifugo moja kwa moja hata kwenye uwekezaji wa miundombinu ya majosho na malisho inakua ni rahisi, lakini sisi wawekezaji sasa tumekuwa na dhana ya kwamba ukitoa takwimu sahihi ya mifugo na kubainika ni mingi labda itakufa au itachukuliwa, niwaambie sio kweli! Jitokeze na takwimu sahihi ili kusaidia uwekezaji wa miundombinu," alisema Dk. Kitambi.

Akisoma hotuba kwa niaba ya mgeni rasmi katika ufunguzi wa mafunzo hayo, Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro, Ezron Kilamhama, aliwataka wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri zote mkoani humo kuhakikisha wanasimamia ipasavyo utambuzi wa mifugo kwa kutumia hereni za kielektroniki.

"Niwaagize wakuu wa wilaya na wakurugenzi kuhakikisha elimu hii inayotolewa leo (jana) inawafikia wafugaji na kuhakikisha mifugo yote iliyoainishwa kwenye mwongozo ambayo ni ng'ombe, punda, mbuzi na kondoo inavalishwa hereni katika maeneo yenu," aliagiza.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Asas, Salim Asas ambaye ni mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) akikata utepe juzi, akizindua rasmi jengo la maabara ya vifaa tiba saidizi katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa, ambalo kampuni yake imejitolea kujenga. PICHA: FRANCIS GODWIN

# Utengenezaji wa viungo bandia waanza Iringa

**Na Francis Godwin,** IRINGA

UTENGENEZAJI wa viungo bandia umeanza kutolewa mkoani Iringa baada ya kampuni ya ASAS Ltd kutoa msaada uliowezesha ujenzi wa jengo la karakana ya kutengeneza viungo hivyo katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa iliyoko mjini Iringa.

Jengo hilo lililozinduliwa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, Salim Asas, limegharimu Sh. milioni 400 zinazojumuisha mashine na baadhi ya vifaa vya kutengenezea viungo hivyo.

Kuanza kutolewa kwa huduma hiyo kumeelezwa na Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Iddy Omary, kwamba kutaleta nafuu kubwa ya gharama kwa wahitaji wa huduma hiyo.

Dk. Omary alibainisha kuwa kabla ya huduma hiyo kuanza kutolewa katika hospitali hiyo, waliokuwa wanahitaji kufanyiwa upasuaji kwa ajili ya kuwekewa viungo bandia walilazimika kutumia gharama za ziada kusafiri kwenda katika hospitali kubwa zaidi ikiwamo Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Hospitali ya Benjamin Mkapa (Dodoma) na hospitali za rufani za kanda; Mbeya na KCMC.

"Hatua hii imepunguza gharama kwa wateja kutoka kati ya Sh. milioni 2.5 hadi zaidi ya Sh. milioni tatu hadi kati ya Sh. 600,000 na Sh. milioni moja. Tunashukuru sana ASAS kwa msaada huu mkubwa," alisema.

Alibainisha kuwa ASAS ilikubali kujenga jengo hilo baada ya kupokea maombi kutoka Hospitali ya Vicensa ya Italia ambayo imeingia ushirikiano na Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa tangu mwaka 2004 kwa ajili ya kuboresha huduma zake.

Mratibu wa Hospitali ya Visenza katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa, Agusto Zambaldo, alisema sekta binafsi na sekta ya umma zinapaswa kuendelea kushirikiana ili kuboresha huduma mbalimbali za afya mkoani Iringa na nchini kwa ujumla.

"Jengo lililoko sasa ni dogo na limechakaa. Nitumie fursa hii kuiomba tena kampuni ya Asas itujengee jengo la mazoezi ili kukamilisha mzunguko wa utoaji wa huduma hii hospitalini hapa," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Bodi yaagiza kampuni kufutiwa zabuni

**Na Happy Severine,**
BARIADI

BODI ya Barabara mkoani Simiyu, imeagiza kufutiwa zabuni kwa kampuni saba za ukandarasi wa usafi wa barabara za lami kwa madai ya kutohudhuria vikao vya bodi mara mbili na badala yake watafutwe makandarasi wengine.

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu ambaye ni mwenyekiti wa bodi hiyo, David Kafulila, alitoa agizo hilo jana wakati wa kikao cha bodi kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Bariadi, mjini hapa.

Kafulila alisema kampuni hizi zimeonyesha dharau kwa kutoshiriki vikao vya kisheria, hivyo hazistahili kufanya kazi ndani ya mkoa na kuagiza Wakala wa Barabara (TANROADS) kuzifutia zabuni na kutangaza upya kwa watu wengine.

Pia wajumbe walisikitishwa na TANROADS kutoa zabuni za usafi wa barabara makandarasi kutoka nje ya mkoa wakati kuna makandarasi wengi wenye uwezo na sifa za kufanya kazi hiyo.

Mbunge wa Itilima, Njalu Silanga, alisema kwa kitendo cha makandarasi hao kutohudhuria vikao hivyo vya kisheria, ni utovu wa nidhani.

Silanga aliongeza kuwa TANROADS ihakikishe zabuni inazozitoa ziwe kipaumbele kwa wazawa ili nao wanufaike na miradi hiyo.

Akiwakilisha taarifa ya wakala, Kaimu Meneja wa TANROADS Mkoa wa Simiyu, John Mkumbo, alisema wanakabiliwa na wizi wa viakisi mwanga 120 ambavyo vimeibwa katika barabara ya Maswa hadi Bariadi. Mkumbo alisema wameshaandika barua na kuipeleka Jeshi la Polisi kuomba wasaidiwe kulishughulikia tatizo hilo.

Naye Meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), Mhandisi Gaston Gasana, alisema kwa mkoa wa Simiyu barabara nzuri ni kilometa 931 sawa na asilimia 22.3 na za wastani ni kilometa 1,720 asilimia 41.3 na mbaya ni kilometa 1,512 asilimia 36.

Mhandisi Gasana aliongeza kuwa kwa mwaka wa fedha 2021/22, TARURA imetia saini mikataba 39 kwa ajili ya matengenezo ya barabara na zaidi ya kilometa 1,080.38 zitafanyiwa matengenezo.



Mwenyekiti wa Chama cha Walimu Mkoa wa Dodoma, Samwel Malecela (kulia), akishiriki chakula cha asili ya kabila la Wagogo kilichoandaliwa kwa ajili ya kuenzi mila na desturí za kabila hilo, hafla iliyofanyika jijini Dodoma juzi. PICHA: IBRAHIM JOSEPH

# Vikundi 3,740 vyaanzishwa kupambana rushwa ya ngono

**Na Sabato Kasika**

KATIKA kupambana na vitendo vya rushwa ya ngono kwa wanafunzi, Shirika la Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI) limeanzisha vikundi 108 vyenye wanachama 3,741.

Vikundi hivyo ni vya madereva wa daladala, bodaboda na bajaj ambavyo vimeanzishwa katika wilaya za Kinondoni, Ilala na Temeke mkoani Dar es Salaam vikiwa na jukumu la kuhamasisha jamii kupinga rushwa hiyo.

Mkurugenzi wa shirika hilo, Janeth Mawinza, alisema hayo jana Dar es Salaam kuwa kaulimbiu ya kampeni hiyo ni 'Safari Salama kwa Wasichana na Wanafunzi Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana'.

Hivi karibuni tulizindua kampeni hiyo wilayani Temeke na sasa kuna vikundi 32 vyenye wanachama 600 ambao ni madereva wa bodaboda, bajaj na daladala," alisema Mawinza.

Alisema madereva hao wanahusika katika kampeni hizo kwa kuwa wao ni kiungo muhimu katika kuvunja rushwa ya ngono kwa kutumia vyombo vyao vya usafiri.

"WAJIKI inaamini kuwa madereva hao pamoja na makondakta wao wakiamua kukataa kuhusika katika rushwa kwa wanafunzi, ukatili wa kijinsia, vitendo vyote vya aina hiyo havitashamiri katika jamii," alisema. Alisema, wao ndio wanaoweza kufuta tabia hizo za kuwarubuni wanafunzi kwa kutumia uhitaji wao, na kwamba WAJIKI inashirikiana nao katika vita hiyo, kwa kuwa wana mchango mkubwa.

Kampeni za shirika hilo, alisema zilianzia katika wilaya za Kinondoni na Ilala tangu mwaka 2018 na sasa zinaendelea kupanuka na zimefika Temeke kuendeleza vita hivyo.

"Katika wilaya za Kinondoni na Ilala, kuna vikundi 72 vya bodaboda na bajaj vikiwa na madereva 2,598 na vikundi vinane vya madereva wa daladala vyenye wanachama 543, kwa ujumla ni wanachama 3,741," alisema.

Mawinza alisema wanafanya kazi hiyo kwa kuwezesha na Taasisi ya Women Tanzania Trust Fund (WTF) na kwamba uwezeshwaji ukiongezeka watafikia wilaya za Kigamboni, Ubungo na hata Tanzania kwa ujumla.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa Shirika hilo, Kalunde Mongomongo, alisema juhudi kubwa zinahitajika kukomesha rushwa ya ngono kwa wanafunzi inayosababishwa na madereva wa bodaboda, bajaj na daladala.

Bahati nzuri WAJIKI imefanikiwa kuhamasisha baadhi ya madereva ambao sasa wana vikundi vyao vinavyofanya kazi ya kuhamasisha wenzao kuwalinda wanafunzi badala ya kuwarubuni," alisema Mongomongo.

Valence Simon, mwenyekiti wa madereva wa daladala Mbagala, alisema yeye na wenzake watashirikiana na shirika hilo kuhamasisha vita dhidi ya rushwa ya ngoni kwa wanafunzi wa kike wilayani Temeke.

Dereva wa bodaboda aliyejitambulisha kwa jina la Maeza Mtoto, kutoka Temeke, alishauri shirika hilo kuendelea kupanua shughuli zake wilayani humo ili kubadilisha madereva bodaboda ambao hurubuni wanafunzi.

# Hatimaye machinga waiangukia h/shauri

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

BAADA ya uongozi wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha kuwaondoa wafanyabiashara wadogo waliokuwa wakifanya biashara kwenye stendi ya zamani ya Maili Moja, baadhi yao wameiangukia halmashauri hiyo iwaruhusu kuendelea na shughuli zao nyakati za jioni.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana, wafanyabiashara hao walisema eneo walilotakiwa waende kwenye soko la Loliondo hakuna biashara kwa kuwa tayari kuna wafanyabiashara wa jumla.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Mwantumu Chedi, alisema walishakwenda katika eneo wanalotakiwa kufanyia shughuli zao lakini biashara kwao imezidi kuwa ngumu huku baadhi yao wakilalamikia mitaji kukata.

Chedi alisema hawapingani na uamuzi wa kwenda kwenye soko la Loliondo lakini kikwazo kilichoko ni kutofanya biashara huku majukumu ya kulea familia yakilegalega.

Naye Nuru Saghire alisema uwapo wao katika stendi ya zamani wateja wao ni watu wanaotoka ofisini na wanawarahisishia kwa kuwa endapo mtu anahitaji mfano chungwa la Sh. 200 hadi afike soko la Loliondo lazima atumie Sh. 2,000 ya bodaboda kwenda na kurudi au 800 akipanda daladala, hivyo wao wanawarahisishia kuwapunguzia gharama.

Shagire alisema walikopelekwa kuna wafanyabiashara wengi, hivyo biashara kwao imekuwa ngumu kuuza bidhaa hali inayosababisha mitaji kupungua.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kibaha, Mhandisi Mshamu Munde, alisema lengo la kuwaondoa wafanyabiashara hao ni kutaka wakae kwenye maeneo yaliyopangwa kisheria na hapo walipokuwa hawako kisheria.

Munde alisema eneo walilokuwa wakifanyia biashara ni hifadhi ya barabara ambayo mali ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS0 ambao wameweka uzuio kwenye stendi ya zamani sehemu ambayo wafanyabiashara hao walikuwa wakiuzia bidhaa zao.

Alisema tayari wafanyabiashara ambao hawakuwa katika maeneo rasmi wamepelekwa kwenye maeneo ambayo ni soko la Loliondo, Sofu, Picha ya Ndege na Lulanzi ambako miundombinu imetengenezwa kwa ajili ya wafanyabiashara.

# Wafugaji wasiosajili mifugo yao sheria kuwabana

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

SERIKALI imesema itawachukulia hatua wafugaji watakaoshindwa kusajili mifugo yao kwa njia ya utambuzi wa hereni za kielektroniki zoezi hilo litakapofungwa Agosti 2022.

Mkurugenzi Msaidizi wa huduma za ukaguzi na ustawi wa wanyama, Dk. Annette Kitambi, alitoa taarifa hiyo wakati wa utoaji mafunzo ya utambuzi wa mifugo kwa kutumia hereni za kielektroniki mkoani Morogoro.

Alisema kwa sasa utoaji elimu unaendelea kwa wataalamu na viongozi kutoka serikali za mitaa ngazi ya mkoa na wilaya pamoja na wafugaji ambao kwa pamoja watahusika katika kutekeleza zoezi hilo linalotarajiwa kuanza mapema Januari mwakani.

"Sheria zipo lakini kwa sasa hivi tunafanya kwa kuwahamasisha na kuwaelimisha, zoezi hili litaenda mpaka Agosti mwakani tutakuwa tumemaliza kwa hiari ndipo sheria zitaanza kutumika na imeweka wazi kwamba ikibainika haijatambulika utapigwa faini ya Shilingi milioni mbili au kwenda jela miezi sita au vyote kwa pamoja," alisema Dk. Kitambi.

Kadhalika aliwataka wafugaji kutoa takwimu sahihi za mifugo wanayomiliki wakati utambuzi wa mifugo kwa mfumo wa hereni za kielektroniki litakapoanza Januari 2022.

Alisema kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya wafugaji ya kutotoa takwimu sahihi za mifugo yao kwa kuhofia kupunguziwa kutokana na wingi wao jambo ambalo limekuwa likikwamisha jitihada za serikali hasa katika ugawaji wa maeneo ya malisho.

"Serikali inapoleta sensa ya mifugo moja kwa moja hata kwenye uwekezaji wa miundombinu ya majosho na malisho inakuwa ni rahisi, lakini sisi wawekezaji sasa tumekuwa na dhana ya kwamba ukitoa takwimu sahihi ya mifugo na kubainika ni mingi labda itakufa au itachukuliwa niwaambie sio kweli tujitokeze na takwimu sahihi ili kusaidia uwekezaji wa miundombinu," alisema Dk. Kitambi.

Akisoma hotuba kwa niaba ya mgeni rasmi katika ufunguzi wa mafunzo hayo, Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Ezlon Kilamhama, aliwataka wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri zote mkoani humo kusimamia ipasavyo utambuzi wa mifugo kwa kutumia hereni za kielektroniki.

Alisema zoezi hilo linaloenda na utoaji elimu kwa watendaji wa serikali ngazi ya halmashauri ni vyema kwa wataalamu kila mmoja akaelewa vizuri mwongozo wa sheria na kanuni ili aweze kwenda kutoa elimu kwa wafugaji na wataalamu walioko ngazi za chini.

"Niwaagize wakuu wa wilaya na wakurugenzi kuhakikisha elimu hii inayotolewa leo inawafikia wafugaji na kuhakikisha mifugo yote iliyoainishwa kwenye mwongozo ambayo ni ng'ombe, punda, mbuzi na kondoo inavalishwa hereni katika maeneo yenu," alisema.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, akimkabidhi pikipiki Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake Tanzania, Wilaya ya Ukerewe, Neema Mgobela, alipotembelea ofisi za UWT Ukerewe jana. **PICHA: HAPPY SHAYO**

## Wanafunzi wakoshwa kukamilishiwa madarasa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANAFUNZI wa kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Mwawaza, Manispaa ya Shinyanga, wamepongeza ujenzi wa vyumba vya madarasa shuleni hapo kwa kuwa yatawawezesha kusoma katika mazingira rafiki na kuepuka msongamano darasani.

Walibainisha hayo jana wakati Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, na Ajira, alipofika shuleni hapo kukagua ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Mmoja wa wanafunzi hao, Winfrida John, alisema wakisoma kwa nafasi wataelewa vizuri masomo na hatimaye kupata ufaulu mzuri na kutimiza ndoto zao.

"Tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kutujengea vyumba vya madarasa shuleni hapa, ambavyo vitaondoa msongamano madarasani na kusoma katika mazingira rafiki na kuelewa masomo yetu vizuri," alisema John.

Naye Mkuu wa Shule ya Sekondari Mwawaza, Juliana Limbe, alisema ujenzi wa chumba kimoja cha darasa shuleni hapo, kunafanya idadi ya vyumba saba na kuondoa upungufu uliokuwapo.

Alisema shule hiyo ina jumla ya wanafunzi 296 na wanatarajia mwakani kupokea 135 kuingia kidato cha kwanza watakaosoma kwa nafasi bila ya msongamano.

Kwa upande wake Mbunge Katambi, akizungumza kwenye ukaguzi wa vyumba hivyo shule za sekondari na shikizi, Manispaa ya Shinyanga, alimpongeza Rais Samia kwa kutoa fedha za ujenzi wa vyumba hivyo na kumaliza tatizo la upungufu wa madarasa shuleni.

Pia alitoa wito kwa wanafunzi kusoma kwa bidii na kupata ufaulu mzuri ili wasimwangushe rais wao ambaye amewaboreshea miundombinu rafiki ya elimu ikiwamo ujenzi wa madarasa.

Katika hatua nyingine, aliwataka wazazi kuwapeleka watoto wao shuleni waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza na kuwatimizia mahitaji yao yote ili wasome na kutimizi ndoto zao, ili baadaye waje kuwa viongozi.

## Waomba kujengewa kituo cha polisi eneo la uwekezaji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

UKOSEFU wa kituo cha polisi katika eneo la uwekezaji maarufu kama 'Dodoma' umesababisha wizi wa mali za wajasiriamali waliowekeza katika eneo hilo na baadhi yao kuuza viwanja na kurejea mjini kufanya shughuli zao kama ilivyokuwa awali.

Eneo hilo lipo Kata ya Zongomela, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, mkoani Shinyanga, likiwa na ukubwa wa hekari 2,100, kati ya hizo 500 zimepimwa zaidi ya viwanja 621 na kuvigawa bure kwa wajasiriamali na hekari 1,600 ilikuwa na wawekezaji wakubwa.

Pia halmashauri hiyo imetoa mikopo kwa vikundi 14 vya wajasiriamali vilivyoko katika eneo hilo kupitia mapato ya ndani kwa zaidi ya Sh. milioni 221, huku kikundi cha kukopeshana (Saccoss) kikipatiwa Sh. milioni 100 na wanaendelea na marejesho ya kurejesha kiwango hicho.

Mwenyekiti wa eneo hilo la uwekezaji, Lenatus Numbi, aliyabainisha hayo jana wakati akizungumza na vyombo vya habari ofisini kwake kuwa, eneo la ujenzi wa kituo cha polisi na taasisi za kifedha lipo, lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa.

Alisema, kituo cha polisi kilichoko kipo umbali wa kilometa tatu kutoka katika eneo la uwekezaji na unapotokea wizi nyakati za usiku inachukua muda polisi kufika na kusababisha wahalifu kutokomea kusikojulikana na mali za wajasiriamali.

Numbi alisema, kituo cha polisi katika eneo hilo kitatoa huduma kwa wananchi walioko katika kata ya Zongomela, Nyahanga, Mhungula, Nyihonga na Kata ya Nyandekwa na kumtaka Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Anderson Msumba kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi kutatua tatizo hilo.

Naye Eziron Ngaiwa alisema, kwa sasa wajasiriamali wanatishia kuuza maeneo yao ya uwekezaji waliyopewa bure na halmashauri na kutumia mjini walipoondolewa kuendelea na shughuli zao na kwamba kama hili lisipotatuliwa hata mikopo waliyopewa watashindwa kuirejesha kwa wakati.

Akijibu hoja hiyo, Meneja wa eneo hilo ambaye ni Ofisa Maendeleo ya Jamii, Hilda Robert, alikiri kutokuwapo kituo cha polisi katika eneo hilo na wameshapokea maombi ya wajasiriamali wa ujenzi wa kituo hicho na muda wowote ujenzi utaanza.

Alisema, wakati wa upimaji wa viwanja na kuvigawa bure kwa wajasiriamali, walitenga maeneo ya ujenzi wa kituo cha polisi pamoja na taasisi za kifedha na hivi karibuni Benki ya Dunia imetoa kilometa 12.6 za ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami na taa katika eneo zima la uwekezaji.

# MISA-TANZANIA yanoa waandishi sheria za habari

**Na Francis Godwin,**
IRINGA

TAASISI ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Jangwa la Sahara (Media Institute of Southern Africa - MISA Tanzania), imekutanisha wanahabari na wadau wa habari mkoa wa Iringa kuwajengea uwezo kuhusu sheria mbalimbali za habari.

Akizungumza baada ya mafunzo hayo, Kaimu Mkurugenzi wa MISA Tanzania, Andrew Marawiti, alisema ni mwendelezo wa mafunzo yanayotolewa kwa wanahabari mikoa mbalimbali ili kuwajengea uwezo wa kutambua na kuchambua sheria hizo na kutoa maoni yao.

Alisema changamoto ni mwitikio kutoka kwa waandishi kujitokeza kupaza sauti kujitetea kuhusu sheria hizo ili ziweze kufanyiwa marekebisho zisiwe mwiba kwa wanahabari na vyombo vya habari.

Alisema lengo kuu la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo waandishi hao ili kutambua maudhui ya sheria hizo.

Pia, kupitia mafunzo hayo waandishi watakuwa na uwezo wa kushiriki mijadala mbalimbali ikiwamo ya mabadiliko ya baadhi ya vifungu katika sheria hizo ambazo zinaonekana kuminya uhuru wa kujieleza.

Mwezeshaji wa mafunzo hayo ambaye ni mwanahabari mkongwe, Jesse Kwayu alisema, kwenye sheria hizo kuna mambo mengi mazuri, lakini mazuri hayo yanafunikwa na vifungu vichache vinavyominya uhuru wa habari na kujieleza.

Kwayu aliwataka waandishi wa habari kuzisoma sheria hizo na kuzielewa ili wawe na uelewa wa vifungu mbalimbali.

"Sheria tulizonazo ukizisoma kwa wepesi utaziona ni nyepesi, lakini ni sheria nzito sana, na mwandishi ili akamilike lazima azifahamu sheria hizi...sheria hizi zipo nyingi, lakini kutokana na utendaji kazi tutajikita katika sheria tatu ambazo ni Sheria ya vyombo vya kielektroniki "EPOCA", sheria ya takwimu "Statistics Act" na Sheria ya vyombo vya habari "Media Service Act 2016," alisema Kwayu.

Alisema sheria hizo zimekuwa zikilaumiwa kuwa zinakinzana na uhuru wa habari kwa mwandishi na lengo kubwa ni kutoa uelewa waandishi wazijue na ipaze sauti ili ziweze kufanyiwa marekebisho kwa ustawi wa tasnia ya habari.

Kwa upande wake mdau wa habari kutoka Asasi ya kiraia ya ICISO mkoani Iringa, Raphael Mtitu, aliwataka waandishi wa habari kushirikisha taasisi za kiraia katika mapambano ya kudai haki ya kujieleza kwa vile ni matakwa ya katiba.

Alisema haki hiyo inamgusa kila mwananchi na ni vyema taasisi zote zikaungana kuipigania.

"Msione hili jambo ni kwenu peke yenu, kama hivi MISA TAN walivyotushirikisha basi iwe fursa kwa taasisi nyingine za habari kuona umuhimu wa kushirikisha taasisi za kiraia ili kuunganisha nguvu na kuwa sauti ya pamoja," alisema Mtitu.

Denis Nyali, kati ya walioshiriki warsha hiyo alisema kuna mambo mengi yanayosonga utendaji wa wanahabari nchini, lakini kwa mara kadhaa waandishi hawatoi ushirikino katika kutatua changamoto za wengine.

Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Iringa (IPC), Frank Leonard, akichangia alisema miongoni mwa sheria zinazokiuka uhuru wa waandishi ni inayo wataka waandishi kuanza kutambulika kuanzia ngazi ya stashahada ya habari na kuendelea.

Washiriki wengine wa mjadala huo walitamani sheria ipitishwe kwa mtu kuwa mbunge lazima awe na kiwango cha elimu kuanzia diploma kama wanahabari ili awe na utashi mkubwa wa kuchambua na kutunga sheria mbalimbali za nchi.

"Wabunge wanapitisha sheria ya kikomo cha elimu kwa wanahabari kuwa ni diploma, wakati ili mtu uwe mbunge kigezo kikubwa ni kujua kusoma na kuandika, ingependeza na wao wabunge kigezo cha elimu kitiliwe mkazo," alisisitiza.



Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi (kulia), akikagua ubora wa sakafu katika ujenzi wa vyumba vya madarasa jana katika Shule ya Sekondari Uzogole Manispaa ya Shinyanga, (kushoto) ni Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Wakumbushwa kufuata sheria matumizi ya maji

**Na Neema Hussein,** KATAVI

WANANCHI wametakiwa kufuata sheria na taratibu wanapohitaji kutumia maji kutoka kwenye vyanzo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwamo kupatiwa kibali na kulipa ada zinazotakiwa ili kusaidia kuleta mgawanyo mzuri kwa kila mtu anayehitaji huduma hiyo.

Akizungumza na baadhi ya waandishi wa habari walioshiriki mafunzo ya utunzaji wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi yaliyofanyika mkoani Kigoma ambayo yalishirikisha waandishi kutoka mikoa ya Kigoma, Rukwa, Tabora na Katavi, Mkuu wa Idara ya Mazingira na Ulinzi Bonde la Ziwa Tanganyika, Injinia Odemba Kornel, alisema maji yanatakiwa yatumike kama rasilimali zingine za nchi zinavyotumika na si bure.

Alisema shughuli ambazo hazihitaji kibali ni maji yanayochotwa kwa ndoo kwa matumizi ya nyumbani au mtu anayechimba kisima kifupi cha mita chini ya 15 na aliyetengeneza tangi la kubeba maji ya mvua ambalo linabeba chini ya lita 20,000.

Kornel alisema utaratibu wa kugawa vibali vya matumizi ya maji kwa shughuli za kumwagilia mashamba, kutengeneza mabwawa ya samaki, kuchepusha mto, kuchimba kisima kirefu, kufua umeme, ni lazima maombi yatumwe na wataalamu waje kukagua na kukushauri matumizi yake.

Alisema Bodi ya Maji pamoja na kuhakikisha wanatunza mazingira na vyanzo vya maji bado kuna tatizo kubwa la vyanzo vyake kuingiliwa kulingana na shughuli za kibinadamu kama vile kunyweshea mifugo, uchimbaji wa mchanga kutoka kwenye mito, upandaji miti pembeni mwa vyanzo, hali inayosababisha maji kupungua kwenye mito au kukauka.

Kwa upande wake, Mhandisi wa Rasilimali za Maji, Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Tanganyika, Gaudens John, alisema miongoni mwa kazi tatu walizonazo ni pamoja na kuyahesabu maji kwa lengo la kusaidia kwenye uamuzi mbalimbali wa shughuli za kiuchumi.

Nipashe ilizungumza na baadhi ya wananchi akiwamo Irene Temu, mkazi wa Manispaa ya Mpanda kujua kama wanazifahamu sheria za matumizi ya maji ikiwamo kuchimba kisima kirefu kwa matumizi ya nyumbani, alisema hajui kama kuna utaratibu wa kupata kibali na kuomba wahusika kuzidi kutoa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi ya rasilimali za maji.

# UVCCM wapewa mikakati ya uanzishaji miradi

**Na Stevie Chindiye,**
TUNDURU

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, Hussein Mkuwia, amewataka vijana wa wilaya hiyo kujipanga na kuunda vikundi vya uzalishaji mali kwa kuanzisha miradi itakayoifanya jumuiya kuondokana na kuwa ombaomba.

Mkuwia alisema hayo wakati akiongea na wajumbe wa Baraza la UVCCM lililofanyika mjini hapa.

Katika taarifa hiyo Mkuwia alipongeza vijana wa kata za Ligoma, Nalasi na Amani kwa kuanzisha mashamba ya pamoja na shamba mradi wa jumuiya yao zikiwa ni juhudi za kujikwamua kiuchumi.

Alisema kwa kufanya hivyo itawasaidia vijana kuondokana na tabia ya kuwa ombaomba kwa viongozi wa kuchaguliwa ili waweze kutimiza majukumu ya kifamilia na hata michango ya chama kupitia jumuiya yao.

Awali, Katibu wa UVCCM, Juma Khatibu, alisema jumuiya inapofikia kipengele cha malipo, chama hukaa pembeni jambo linaloileta malalamiko.

"Yapo mambo mengi ambayo hutokea kwa mfano unapanga bajeti ya Sh. milioni 10 kulingana na mahitaji, lakini inapopelekwa chama hakitoi fedha yote," alisema Khatibu.

Katika taarifa hiyo, Khatibu alisema Jumuiya ina wanachama hai 28,466 wakiwapo wakawake 11,206 na wanaume 17,260.

Akizungumzia usajili wa wanachama kupitia mfumo wa kielektroniki, alisema waliosajiliwa wapya ni 4,007 wakiwamo wanawake 1,206 na wanaume 2,801.

Kwa upande wake Katibu wa hamasa wa Jumuiya hiyo, Yanini Stambuli, aliwataka vijana kujitokeza kuwania nafasi za uongozi ndani ya chama kwa kuwa kipindi hicho kikifika hakuna kiongozi mwenye hatimiliki katika chama hicho.

Wakiongea kwa nyati tofauti baadhi ya wajumbe wa mkutano huo walilalamikia utaratibu wa kuwafanyisha kazi hasa kipindi cha uchaguzi na kutowalipa stahiki zao jambo ambalo limekuwa likizua mang'uniko miongoni mwao.





Ukurasa 14

NI ZAIDI YA MSIBA, KIFO CHA ASKOFU TUTU



Ukurasa 13

## Mwaka uliojaa simanzi, faraja miradi mikubwa ya maendeleo

siasa
JUMATANO DESEMBA 29, 2021
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

MATUKIO YALIYOITIKISA BONGO 2021

# Kilio miamala, wabunge 19 CHADEMA, ukame, corona, katiba, tume huru uchaguzi

**Na Waandishi Wetu**

TUNAWATAKIA wasomaji wetu heri ya Mwaka Mpya wa 2022, tunawakaribisha tena kuendelea kusoma Kijarida cha Siasa, ili kupata makala mbalimbali zinazosisimua na kuelimisha.

Tunapouaga mwaka 2021, ni mwaka uliokuwa na habari mbaya za vifo vya viongozi akiwamo Rais wa awamu ya tano, John Magufuli, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad na Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. John Kijazi.

Aidha, ulichukua maisha ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Elias Kwandikwa, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji, William Ole Nasha, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mhandisi Patrick Mfugale.

Umekuwa mwaka wa tozo, ulioanzisha manung'uniko ya wananchi kuhusu uamuzi wa bunge wa kupitisha tozo mbalimbali zikiwamo za miamala ya simu, laini pamoja na kodi za majengo, malipo yanayofanywa kupitia LUKU wakati wa kununua umeme.

Kukatika umeme mara kwa mara ingawa inaelezwa kuwa hakuna mgawo, tishio la ukame karibu nchini nzima na mvua kuchelewa.

Kadhalika kuanza mgawo wa maji ya bomba mijini ikiwamo Dar es Salaam ni mambo yanayouhusu mwaka huu.

Mwaka 2021 umekuwa wa kwanza kwa Tanzania kuagiza chanjo ya ugonjwa wa corona ambao ulikuwa ni tishio kwenye baadhi ya mikoa hasa Kilimanjaro, Arusha na Kanda ya Ziwa.

Aidha, maamuzi ya bunge kupitisha tozo, ni eneo ambalo limeleta manung'uniko, zipo tozo za laini ya simu, miamala



Rais John Magufuli alipokula kiapo kuiongoza Tanzania Novemba 2020, baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba. **PICHA: MTANDAO**

ya kutuma na kupokea fedha na kulipa kodi ya majengo kupitia malipo ya umeme.

Kukatika kwa umeme kila mara ingawa inaelezwa kuwa hakuna mgawo wa nishati hiyo nchini, ulitishia kwa kiasi kikubwa.

Aidha, kuwapo na ukame karibu nchini nchi nzima na mvua kuchelewa hadi Novemba ni miongoni mwa yaliyojiri. Kadhalika baadhi ya maeneo kupata mgawo wa maji ya bomba huku corona ikitishia kwenye baadhi ya mikoa hasa ya Kilimanjaro, Arusha na Kanda ya Ziwa ni mambo ya kukumbukwa.

### KUTUNISHIANA MISULI

Katika uwanja wa siasa mwaka 2021, umeshuhudia suala na mivutano kati ya Msajili wa Vyama vya Siasa na wadau wa siasa wakiwamo viongozi wa vyama vya upinzani hasa kwenye suala la kuruhusu mikutano ya vyama hivyo.

Mvutano huo uliibuka baada ya Msajili kuandaa mkutano ili kujadili sintofahamu uliopo kati ya vyama vya upinzani na Jeshi la Polisi kufuatia polisi kukusanyika kwa wingi katika mikutano ya vyama hivyo hata ya ndani na mara nyingine kuikataza. Mkutano huo ulikuwa ufanyike Oktoba 2021 jijini Dodoma.

Baadhi ya vyama viligomea mkutano huo, vikidai kuwa polisi hapaswi kuwapo kwenye mkutano huo, kwa madai kwamba wao wanatumwa kutekeleza tu, hivyo alihitajika Waziri wa Mambo ya Ndani.

Hiyo ilikuwa ni kauli ya Chama cha ACT-Wazalendo, huku CHADEMA kikiweka masharti kuwa hadi mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe, anayekabiliwa na kesi ya ugaidi aachiwe huru bila masharti, ndipo kingeshiriki.

NCCR-Mageuzi, wao walidai

INAENDELEA UK.12

# Kilio miamala, wabunge 19 CHADEMA, ukame, corona, katiba, tume huru uchaguzi

INATOKA UK.11

kuwa hawawezi kuhudhuria mkutano huo, kwa kuwa hauna jipya bali kinachotakiwa ni msajili kufuata sheria ya vyama vya siasa badala ya kuitisha mkutano kwa jambo ambalo lipo wazi.

Mvutano huo ulisababisha mkutano huo kuahirishwa hadi mwanzoni mwa Desemba, ulipoitishwa na kufunguliwa na Rais Samia Suluhu Hassan huku baadhi ya vyama vilivyokuwa vimesusia vikahudhuria.

ACT-Wazalendo ni miongoni mwa vyama vilivyokuwa vimesusa lakini vikahudhuria, huku NCCR-Mageuzi na CHADEMA vikiendelea na msimamo ukiwamo wa kutaka Mbowe kuachiwa huru.

Aidha, suala la kesi Mbowe limekuwa miongoni mwa mambo ambayo yameshika kasi kwenye mitandao ya kijamii kwa mwaka huu, huku likifuatiliwa na watu wa kada mbalimbali nje na ndani ya nchi.

**MAAZIMIO YALIYOFIKIWA**

Baada ya kutunishiana misuli kati ya vyama vya upinzani na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa vile ambavyo hatimaye vilihudhuria mkutano, vilitoka na maazimio ambayo yaliwekwa hadharani.

Mkutano wa Msajili wa Vyama vya Siasa na wadau walipitia maazimio 80, miongoni mwake yakiwa ni suala la katiba mpya, kwamba, badala ya kuendelea na mchakato wa katiba mpya, yachaguliwe mambo machache yanayolalamikiwa sana na kuanza nayo.

Kwa maana hiyo, katiba mpya imeendelea kuwa kiporo, lakini Rais alishaombwa aachwe aimarishe uchumi kwanza, ingawa imekuwa ikielezwa kuwa suala la katiba mpya halikwepeki.

CUF nayo ilishasisitiza kuwa haitashiriki uchaguzi wowote hadi hapo katiba mpya na tume huru ya uchaguzi vitakapopatikana, ingawa katika maazimio, wadau wanatakiwa kuongeza imani kwa watendaji na viongozi wa tume iliyopo.

Wadau hao walikubaliana pia kufanyika kwa mapitio ya sheria ya vyama vya siasa, mchakato uwe shirikishi na pia kupitia Sheria ya Jeshi la Polisi ili liwe na weledi na kuondoa uonevu unaofanywa kwa kisingizio cha kutekeleza sheria.

Vilevile walikubaliana kufuata katiba, sheria, kanuni na miongozo katika kutekeleza majukumu yao, na kwamba vyombo vya maamuzi vina wajibu wa kutenda haki na kulinda amani, kwa kuwa msingi wa amani ni haki.

**KIPORO WABUNGE CHADEMA**

Wabunge 19 wa CHADEMA, walioapishwa kupitia utaratibu wa viti maalumu wameendelea kuwa wabunge na kushiriki vikao vya bunge licha ya chama hicho kudai kuwa ni kinyume na msimamo wao kwa vile kufanya hivyo ni kuhalalisha Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28 mwaka 2020, wakidai haukuwa huru na haki.

Hadi sasa mwaka 2021 unapomalizika hatima ya wabunge 19 wa viti maalumu ambao awali walifukuzwa uanachama CHADEMA na kupinga kwa kukataa rufani Baraza Kuu la Chama, haijafahamika.



Halima Mdee (kushoto), mmoja wa wabunge 19 wa viti maalumu wa CHADEMA, aliyevuliwa uanachama, lakini Baraza Kuu la CHADEMA halijatoa maamuzi kuhusu hatima yao. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> "Ni vizuri mchakato wa kuunda na kuwa na katiba mpya, uanzie ngazi za awali kwa kuendesha mafunzo na kampeni kwa wananchi kuisoma katiba ya sasa na kuielewa.



Jaji Francis Mutungi, Msajili wa Vyama vya Siasa.

**DARASA LA POLEPOLE**

Mwaka 2021 limeibuka darasa la uongozi kwenye mitandao ya kijamii lililoanzishwa na aliyewahi kuwa Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Taifa, Humphrey Polepole, ambalo limezua mjadala.

Darasa hilo limeibua watu wa kada mbalimbali kila mmoja akiwa na lake, wakiwamo wanaompinga na kuhoji kwamba, alikuwa wapi kuanzisha darasa hilo na wengine kumuunga mkono kuwa ana haki ya kutoa maoni yake.

Hata hivyo mwanasiasa huyo amezuiwa kuendelea na darasa hilo la uongozi na sasa hakuna mijadala tena ambayo ilikuwa ikisababishwa na darasa hilo aliloanzisha baada ya kutoka nafasi ya uenezi.

Wapo ambao hawakuvumilia darasa hilo na kuamua kumvaa hadharani akiwamo kada wa CCM, Abdalah Bulembo aliyemtaka mwanasiasa huyo aiache serikali itekeleze majukumu yake.

Aidha, kuliibuka pia malumbano kutoka kwa baadhi ya wabunge wa CCM dhidi ya uamuzi wa serikali wa kutaka watu kupata chanjo ambapo wengine walikuwa wakipinga hadharani kuwa hawatachanja.

**KATIBA MPYA**

Suala la katiba mpya na kuwapo kwa tume huru ya uchaguzi ni moja ya mambo yaliyozungumzwa sana mwaka huu.

Baadhi ya watetezi wakuu wa katiba hiyo ni Waziri Mkuu mstaafu Joseph Warioba, anayesema ni hitaji la Watanzania kwa sasa na haikwepeki.

Pamoja na Warioba, viongozi wa dini, wasomi na asasi za kiraia zimezungumzia suala la kuandikwa katiba mpya itakayolingana na matakwa ya sasa ya siasa za vyama vingi.

Mwenyekiti wa CUF Taifa, Profesa Ibrahimu Lipumba ni miongoni mwa watetezi wa kuwapo kwa tume huru ya uchaguzi.

Anatangaza msimamo huo tangu mwanzoni mwa mwaka huu kuwa CUF itakuwa na jukumu moja pekee la kuhimiza kutayarishwa tume huru ya uchaguzi na bila kuwapo haitashiriki uchaguzi mkuu.

**KATIBA MPYA YA NINI?**

Wakati mwaka huu unaelekea ukingoni NIPASHE imezungumza na mwanachama na mmoja wa viongozi wa zamani wa Chama cha NCCR- Mageuzi, Fautine Singura ambaye anadai kwamba katiba ya wananchi au ya Jaji Warioba, inayopigiwa chapuo haifai.

Kwa nini? Anadai kuwa iliandaliwa kwa jazba, chuki, haraka na ina mapungufu mengi na mchakato wa kupata katiba mpya, unahitaji taifa kujipanga, kuweka hadidu za rejea na muda wa kupata katiba hiyo.

Sungura anaamini kwamba, wanaotaka katiba ya Warioba hawajawahi kuisoma wala hawaifahamu.

"Ni vizuri mchakato wa kuunda na kuwa na katiba mpya, uanzie ngazi za awali kwa kuendesha mafunzo na kampeni kwa wananchi kuisoma katiba ya sasa na kuielewa," anasema Sungura.

Anafafanua kuwa baada ya kuisoma, wanatakiwa kukizungumzia wanasichokitaka ili kiondolewe, wachokitaka kwenye katiba mpya wanayoiandika, na kwamba ni muhimu kuisoma iliyopo ili wajue ni wapi pa kurekebisha, kufuta pa kuweka mambo mapya, na kwamba kazi hiyo inaweza kuchukua kati ya miaka minne hadi saba."

Anakumbusha Sungura kuwa Watanzania wanapotaka katiba mpya, wanatakiwa kufikiria uwezekano wa kuwa na katiba inayodumu kwa miaka 50 hadi 100, na anatolea mfano Kenya, kwamba, waliandika katiba mpya, lakini ndani ya kipindi cha miaka mitatu wanatakiwa tena kuifanyia marekebisho.

**MAREKEBISHO MUHIMU**

"Katiba ya Tanzania inahitaji kufanyiwa marekebisho, kwa mfano rais anapofariki, makamu wake anachukua nafasi. Vipi ikitokea wote wawili wamefariki ni nani anachukua nafasi ya uongozi wa taifa?

Tunawatakia wasomaji wetu heri ya mwaka mpya 2022 . Tukutane tena Jumatano Januari 5, 2022.

KWA HERI 2021

# Mwaka uliojaa simanzi, faraja miradi mikubwa ya maendeleo

Na Sabato Kasika



Rais Samia Suluhu Hassan akila kiapo. **PICHA: MAKTABA**

WAKATI mwaka 2021 unafikia ukingoni, unaondoka ukiwa umeiachia Tanzania matukio mengi makubwa, mojawapo likiwa ni la kufariki kwa aliyekuwa Rais wa awamu ya tano, Dk. John Magufuli, wasaidizi wake Katibu Mkuu Kiongozi John Kijazi, lakini Zanzibar Makamu wa Kwanza Rais, Seif Sharif Hamad.

Kwa mara ya kwanza kifo cha Magufuli, kiliandika historia upande wa Tanzania Bara, Rais kufariki akiwa madarakani, tukio hilo likitokea miaka 49 baada ya kifo cha Abeid Amani Karume, aliyeuawa mwaka 1972 akifariki dunia akiwa madarakani.

Kwa upande mwingine 2021 umefungua tena ukurasa mpya wa historia ya taifa kuongozwa na Rais mwanamama tangu kupata uhuru mwaka 1961, Samia Suluhu Hassan.

Licha ya Magufuli kuondoka ameiachia nchi historia ikiwa ni pamoja na kuimarisha mifumo ya kukusanya mapato ya serikali wa GePG na kuanzisha utaratibu wa kulipa kimtandao.

**UJIO KONTROLI NAMBA**

GePG ni kifupisho cha "Government e-Payment Gateway System" ambao ni mfumo wa kielektroniki (unaotumia kompyuta) unaowezesha kukusanya fedha za umma kupitia simu za mkononi na mawakala pamoja na benki uliobuniwa na kutengenezwa na wataalamu wa Tanzania ambao unawawezesha wananchi kulipia huduma mbalimbali za serikali kupitia mfumo huo wakitumia 'kontroli namba.'

Ukusanyaji huo mapato ya ndani umewezesha wananchi kuwa na uhakika wa malipo mbalimbali yanayofanyika kupitia kontroli namba ambayo ni salama zaidi katika mchakato wa ukusanyaji na uwasilishaji pesa serikalini.

Mfumo huo ulioanzishwa mwaka 2017 na serikali ya awamu ya tano umeunganishwa na taasisi mbalimbali za serikali za mitaa, halmashauri, taasisi na serikali kuu ambapo umewezesha kuongezeka kwa mapato na kuiwezesha serikali kutekeleza shughuli zake mbalimbali ikiwamo kuimarisha utoaji wa huduma kwa jamii na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Kuna baadhi ya maeneo malipo ya serikali hufanyika kwa risiti za mikononi mfano stendi ya Mbezi watumishi wa Wakala wa Barabara wa Taifa (TANROADS) hukusanya fedha mikononi inapokuja 2022 watumie mfumo wa GePG.

**MIRADI YA UMEME**

Kwenye suala la umeme, Magufuli alidhibiti mgawo na alitamani kuona nchi nzima inakuwa na nishati hiyo kuanzia mijini hadi vijijini, akawa anafuatilia kwa umakini miradi yote ya umeme, ili kuhakikisha inajengwa na inakamilika kwa wakati.

Awamu ya tano ilikuta kituo cha kuchakata umeme wa gesi wa Kinyerezi I, alikamilisha na kinazalisha umeme wa megawati 335, na kujenga kingine cha Kinyerezi II kikizalisha megawati 240 na Kinyerezi III megawati 600 ambacho kinaendelea kujengwa.

Alipohutubia bunge baada ya kushinda uchaguzi kwa ajili ya kuongoza nchi katika kipindi cha pili, aliainisha vipaumbele katika sekta ya nishati kwamba serikali yake ilijipanga kufikisha umeme katika vijiji vyote ambavyo bado havijafikiwa na ni nishati hiyo.

Katika ufafanuzi wake alisema havizidi vijiji 2,384, na kwamba alikuwa ameshafikisha nishati hiyo katika vijiji 9,884 kutoka 2,018 alipoingia ikulu mwaka 2016, huku akibainisha kuwa nchi ina jumla ya vijiji 12,280.

Ili kufanikisha hilo, alipanga pia kuimarisha miundombinu ya nishati na kuboresha upatikanaji wa huduma za umeme nchini na alikuwa amekusudia kukamilisha ujenzi wa bwawa la kufua umeme wa maji wa Nyerere lenye uwezo wa kuzalisha megawati 2,115 sambamba na kuanza ujenzi wa miradi mingine mipya ya umeme wa maji katika maeneo mbalimbali ukiwamo wa Rufiji ili kupata megawati 358.

Kadhalika mradi mwingine ni wa Rumakali unaotarajiwa kuzalisha megawati 222, Kikonge megawati 300, umeme wa gesi asilia Mtwara wa megawati 300, Somanga Fungu wa megawati 330 na Kinyerezi IV wa megawati 300 na mingine midogo.

**FUNZO**

Licha ya kwamba Magufuli ameondoka kazi hizo zimebaki kuwa majukumu ya TANESCO hata sasa, lakini ambacho taifa linajifunza na kuendelea kukienzi ni kwamba Tanzania inakua kila siku. TANESCO inapata wateja wapya kuanzia nyumbani, mabweni, hospitali, shule, viwanda, ofisi na kampuni. Yote hayo yanahitaji kuwa na uwekezaji mpya kila wakati hivyo, ni lazima kila mwaka kuwe na ongezeko la umeme kwenye gridi ya taifa, uwe wa maji, jua, gesi na maji kwa vile wateja wanaongezeka kila uchao. Hivyo juhudi ziongezwe kuongeza umeme kila mwaka kwenye gridi ya taifa.

Mbali na hayo, alikusudia kuzalisha umeme megawati 1,100 kwa kutumia nishati jadidifu ambayo ni jua, upepo na jotoardhi, lakini kukamilisha mradi wa kusafirisha umeme wa msongo wa kilovolti 400 umeme huo ni kutoka Singida kwenda Arusha hadi Namanga na mwingine unaoanzia Iringa kwenda Mbeya hadi Tunduma kwa ajili ya kuunganisha Tanzania na nchi jirani za Kenya na Zambia.

**HAKUNA KESI UCHAGUZI**

Rais Magufuli ameondoka akiwa ameokoa fedha za walipa kodi katika uchaguzi mkuu wa mwaka jana, kwani pamoja na CCM kushinda viti vingi vya udiwani na ubunge, hakuna kesi mahakamani ya kupinga matokeo ya uchaguzi huo.

Hatua hiyo ya kutokuwapo kwa kesi, ni wazi kwamba itakuwa imeokoa fedha nyingi za walipa kodi, kutokana na ukweli kwamba, kubatilisha na kurudia uchaguzi katika kata moja gharama yake inaweza kufikia Sh. milioni 200.

> Katika ufafanuzi wake alisema havizidi vijiji 2,384, na kwamba alikuwa ameshafikisha nishati hiyo katika vijiji 9,884 kutoka 2,018 alipoingia ikulu mwaka 2016, huku akibainisha kuwa nchi ina jumla ya vijiji 12,280.

Kwenye uchaguzi wa jimbo, gharama yake inaweza kufikia Sh. bilioni moja, sasa kwa kata na majimbo yaliyoko nchini, kama kesi za kupinga matokeo zingefunguliwa zikatenguliwa, uchaguzi ungerudiwa na gharama zingekuwa kubwa zaidi.

Kama kesi zingekuwapo baadhi ya matokeo yakafutwa, zingeifanya nchi kutumia fedha nyingi ambazo zilipaswa kuelekezwa kwenye miradi mingine ya maendeleo ikiwamo ya umeme, huduma za afya na elimu.

Hivyo ni wazi kwamba ameondoka akiwa ameokoa fedha kupitia uchaguzi mkuu, ambao huenda wanasiasa walikubaliana na matokeo au hawakuwa na fedha za kuendesha kesi mahakamani.

Lakini kwa ujumla ni kwamba, kutokuwapo kesi za kupinga uchaguzi huo ambao kwa mara ya kwanza tangu kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi CCM mwaka 1992 ilishindwa majimbo mawili tu, ni wazi fedha zimeokolewa.

Ujenzi wa barabara za vijijini na mijini na kukabiliana na uchakavu haraka iwezekanavyo ni jambo alililoanzisha Magufuli baada ya kuunda Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA). Wakala huyo aliondoa ufanyaji kazi wa kimazoea uliokuwa unafanywa na wahandisi wa halmashauri ambao walizitelekeza na kuzisahau barabara na madaraja ya vijijini, lakini kupitia kazi hiyo 'hakuna kulala.'

JUKWAA LA VIONGOZI



Askofu Desmond Tutu na Nelson Mandela baada ya uhuru wa Afrika ya Kusini. **PICHA: MTANDAO**

# Ni zaidi ya msiba, kifo cha Askofu Desmond Tutu

- Kinara kupinga ubaguzi wa rangi, msema kweli
- Aliwasuta Mugabe, Uingereza na Wayahudi

**Na Michael Eneza**

MAOMBOLEZO nchini Afrika Kusini kufuatia kifo cha Askofu Mkuu mstaafu wa Jimbo la Johannesburg, Kanisa la Anglikana, Desmond Tutu, ni zaidi ya kuondokewa na mhamasishaji na mfariji wa kipekee nchini humo.

Umekuwa pia ni muda wa taifa hilo kujitazama kwenye kioo kuona imefikia wapi na maadili aliyoyasimamia Askofu Mkuu Tutu, ndani ya mawimbi kadhaa yanayopingana nchini humo. Si rahisi kusema kinachoonekana kinapendeza, ila kiliboreshwa na juhudi za hayati Tutu.

Askofu Mkuu huyo alifariki akiwa na umri wa miaka 90, wafuatiliaji habari wanasema ni miezi takriban miwili iliyopita alikuwa akisherehekea siku ya kuzaliwa, hali ambayo inakumbushia jinsi hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, alivyofikia kifo chake.

Hakuwa na kawaida ya kila wakati ya kusherehekea siku ya kuzaliwa, ila alipofikia miaka 75 alifanya hivyo, halafu kukawa na mazingira ya ziada, kuwa mama yake mzazi alifariki wakati huo, na yeye akaondoka duniani baada ya miaka miwili huyo ni Nyerere.

Ila kwa Askofu Tutu sherehe ilifuatiwa na kifo, miezi miwili tu, baada ya kufikisha miaka 90.

**KUPINGA UBAGUZI**

Askofu Tutu anabaki kuwa mmoja wa mashujaa wa harakati kupinga ubaguzi wa rangi Afrika Kusini, licha ya kwamba

> “Hata hivyo, wapo baadhi wanaomchukulia kuwa alikuwa na nia nzuri lakini iliikwamisha Tanzania kimaendeleo, kiuchumi, kisiasa na kidemokrasia kama ambavyo ilitokea ya mataifa ya Afrika.



mwaka 2010, aliposherehekea miaka 79 ya kuzaliwa kwake, alitangaza kustaafu kutoka shughuli za umma.

Mzee Tutu alisema anatoa nafasi kwa vizazi vipya kuongoza. Katika harakati zake kupinga ubaguzi wa rangi Askofu Tutu alihudumu pia kama askofu mkuu wa jimbo la Cape Town na baada ya uhuru wa Afrika Kusini akateuliwa kuongoza Tume ya Haki na Maridhiano.

Tume hiyo ilichunguza uhalifu uliotekelezwa katika enzi ya ubaguzi wa rangi. Mwaka 1984 mtetezi huyo wa haki za kibinadamu akashinda Tuzo ya Amani ya Nobel na kwa wengi ni msingi wa maadili katika jamii. Katika huduma yake akiwa Askofu wa Kiangilikana miaka ya 70 Mzee Tutu alikuwa sauti iliyopinga ubaguzi wa rangi.

Alitunukiwa tuzo ya Nobel mwaka 1984 kwa jukumu lake katika mapambano ya kukomesha mfumo wa ubaguzi wa rangi na kudumisha amani na upendo.

Kampeni zake dhidi ya utawala wa makaburu aliipeleka katika makazi ya Waafrika miaka ya 80 na alisimamia haki na kuheshimu ubinadamu na katika tukio moja aliwatuliza na kuwakataza raia waliokuwa na hasira wakitaka kumteketeza polisi Mzungu na kuokoa maisha yake.

Japo amefariki dunia na pia amejiondoa kwenye masuala ya kisiasa, Desmond Tutu anabakia kuwa mfano wa kujivunia nchini Afrika Kusini na kiongozi wa kuigwa barani Afrika.

Tutu alishiriki katika vita dhidi ya ubaguzi wa rangi akishirikiana na Nelson Mandela, na kuchochea harakati za kukomesha sera ya ubaguzi wa rangi iliyofanywa na Wazungu dhidi ya Weusi walio wengi nchini Afrika Kusini kuanzia mwaka 1948 hadi 1991 na kifo chake kinajiri miezi michache baada ya Rais wa mwisho wa enzi za ubaguzi wa rangi Frederik Willem de Klerk, kufariki akiwa na umri wa miaka 85.

Tutu alianzisha jina la Taifa la Rainbow kuelezea mchanganyiko wa watu wa makabila, rangi na dini tofauti nchini Afrika Kusini. Ikiwa ni kuonyesha njia ya kupinga ubaguzi wa rangi.

Desmond Tutu aliyezaliwa mwaka 1931 katika mji mdogo wenye migodi ya dhahabu wa Transvaal alikuwa mwaminifu kwa nafsi yake, taifa na Mungu wake ambaye hakuogopa kusema ukweli.

**MSEMA KWELI DAIMA**

Alikuwa haogopi, alikuwa anasema lile aliloona ni la kweli na kama haki ilikosekana kwa wanadamu hakukaa kimya, kwa mfano alimshambulia Rais Robert Mugabe kutokana na siasa zake na mikakati iliyovuruga uchumi.

Aidha, alikuwa na sauti kubwa katika kumshutumu Robert Mugabe, wakati mmoja alimwelezea kama “mchoro wa katuni wa dikteta wa zamani wa Kiafrika”. Mugabe, kwa upande wake, alimtaja Tutu kama “mwovu”.

Mara nyingine angeweza pia kuwa mkosoaji wa kanisa lake la Kianglikana hasa baada ya mzozo wa kuwekwa wakfu kwa maaskofu mashoga, akipinga maelekezo hayo.

Hakuishia kumkosoa hadharani Mugabe alimkosoa hata aliyekuwa Waziri Mkuu Uingereza, mwaka 1989, alipokwenda mjini Birmingham nchini Uingereza, alikosoa kile alichokiita “nchi mbili” Uingereza, na kueleza kushangazwa na kuwapo watu weusi wengi katika magereza ya nchi hiyo na kutaka haki itendeke.

Hakuwakalia kimya Waisraeli na Wapalestina, aliwakasirisha Waisraeli wakati wa hija ya Krismasi kwenye ardhi hiyo takatifu, akiwalinganisha Waafrika Kusini weusi na Waarabu katika ukingo wa magharibi na Gaza unaokaliwa kwa mabavu na Waisraeli, akisema hawezi kuelewa ni vipi watu walioteseka kama Wayahudi wangeweza kuwasababishia Wapalestina mateso hayo, leo.

Mtaalamu mmoja akiandika kwenye ukurasa wa gazeti na makala ikachapishwa nchi kadhaa duniani anahoji wakati wa maombolezo ya Askofu Tutu kama utawala wa kidemokrasia utaendelea kuwapo Afrika Kusini katika miaka 25 ijayo?

Tatizo la uchambuzi wa mwanazuoni huyo anayetumia jina la Profesa Balthazar ni kuwa yeye pia amejikita katika mwelekeo dhaifu wa kimaadili ukilinganisha na Mandela na Tutu, ila kwa upande fulani unaendana na mrithi wa Mandela, Rais mstaafu Thabo Mbeki. Anasema badala ya kupiga hatua ‘kuelekea taswira ya kinachotufanya tuwe Waafrika, nchi imegubikwa na ukereketwa wa kizalendo unaobomoa taifa, dola kujidai kufuatilia mabadiliko kumbe ni kutaka umiliki wa sekta za kiuchumi, kushamiri mno ukosefu wa ajira na umaskini.’ **MITANDAO**





# Mil. 250/- tozo simu kujenga kituo cha afya

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma, imepokea Sh. milioni 250 zinazotokana na tozo za miamala ya simu kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Chitego.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Dk. Omary Nkullo, alibainisha hayo juzi alipokuwa amefuatana na maofisa kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kukagua maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho.

Alisema mbali na Kata ya Chitego kuwa eneo la kimkakati kutokana na shughuli za kiuchumi na uwepo wa watu wengi, kwa huduma za afya wananchi wake walikuwa wanazifuata mbali.

Vilevile alisema Kata ya Chitego ilikuwa haina kabisa kituo cha afya, hivyo kusababisha watu kufuata huduma za afya katika hospitali ya wilaya takribani kilometa 100.

"Na kwa kituo cha afya cha jirani ni zaidi ya kilometa 40 ambacho kiko kata ya Mkoka. Naishukuru ya serikali kwa kutupatia fedha hizi za tozo za miamala ya simu ambazo ni mkombozi kwa wananchi wa Kata ya Chitego kwa kupata kituo cha afya kama ambavyo kata hii iko pembezoni mwa mpakani mwa Mkoa wa Manyara," alisema.

Diwani wa Chitego, Peter Kalunzu, alisema wamepata changamoto nyingi ikiwamo wajawazito kujifungua njiani kutokana na kufuata huduma mbalimbali za hospitali.

Alisema ujenzi wa kituo cha afya katika kata hiyo utawasaidia wananchi kupata huduma kwa karibu na kupunguza vifo vya watoto wachanga na wajawazito.

# Dodoma yajizatiti katika kupambana na UVIKO- 19

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKOA wa Dodoma unaendelea kutekeleza mikakati ya kukabiliana na ugonjwa wa UVIKO-19 ikiwamo kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa uhakika wa dawa, vifaa tiba na mitungi ya hewa ya oksijeni na viunganishi vyake katika vituo vya kutolea huduma.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Best Magoma, alibainisha hayo jijini Dodoma kwenye taarifa yake aliyoiwasilisha katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC).

Dk. Magoma alisema mikakati mingine ni pamoja na halmashauri, hospitali za kanda na mkoa kuendelea kuchukua tahadhari za kujikinga na maambukizi katika sehemu za kutolea huduma na kuhimiza unawaji wa mikono kwa maji tiririka na sabuni, matumizi ya vipukusi na uvaaji wa barakoa.

"Halmashauri kuimarisha usimamizi wa utekelezaji afua za kujikinga na magonjwa ya mlipuko hususani unawaji wa mikono kwa maji tiririka na sabuni katika maeneo ya umma, taasisi kama vile vyuo, shule, makanisa, masoko na kuepuka misongamano isiyo ya lazima," alisema Dk. Magoma.

Kuhusu huduma za chanjo ya UVIKO-19, alisema mkoa ulipokea dozi 50,000 za chanjo na Agosti 3, 2021 mkoa ulizindua kampeni ya uchanjaji na hadi kufikia Oktoba 5, 2021 chanjo zote zilikuwa zimeisha.

"Kutokana na hali hiyo, mkoa ulilazimika kuomba chanjo za ziada 6,515 kutoka mikoa ambayo uchanjaji ulikuwa chini na walikuwa na shehena kubwa ya chanjo ambako mkoa wa Geita tulipata dozi 5,000 na Iringa dozi 1,515," alisema.

Pia alisema hadi Oktoba, mwaka huu, watu waliochanjwa walikuwa 52,599 kwa chanjo aina ya Johnson & Johnson (JJ) na dozi zote zimekwisha.

Sambamba na hilo, alisema mkoa umepokea dozi 50,390 za chanjo ya UVIKO-19 aina ya Sinopharm ili kuendelea na utoaji wa chanjo kwa wananchi.

"Hali ya uchanjaji ni kama ifuatavyo Dodoma Jiji waliochanja ni 17,831, Chamwino 6,767, Kongwa 5,554. Kondoa 5,472, Mpwapwa 4,869, Chemba 4,389, Bahi 4379 na Kondoa Mji ni 3,338," alisema Dk. Magoma.

Akizungumzia hali ya lishe, alisema Dodoma ni miongoni mwa mikoa yenye tatizo kubwa la utapiamlo hasa kwa wanawake walio katika umri wa kuzaa na watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

"Takwimu zinaonyesha Dodoma ina asilimia 37.2 ya watoto waliodumaa (TNNS 2018). Pamoja na juhudi zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa lishe za kupunguza baadhi ya changamoto za utapiamlo bado jitihada zaidi zinahitajika," alisisitiza, Dk. Magoma.



Mke wa Waziri Mkuu mstaafu, Tunu Pinda, akimvalisha begi la shule mmoja wa watoto wanaoishi katika mazingira magumu kwa ajili ya maandalizi ya shule kwenye hafla iliyoandaliwa na Kanisa la Upendo Revival Christian Center (TAG), Area D jijini Dodoma, iliyofanyika mwishoni mwa wiki. (Kulia) Mchungaji Kiongozi wa kanisa hilo, Askofu Dk. Vangast Salumu. PICHA: PETER MKWAVILA

# Wahamiaji haramu wanaswa ndani ya lori

**Na Renatha Msungu,** KONDOA

JESHI la Polisi wilayani Kondoa, limewatia mbaroni wahamiaji haramu 51 waliokuwa wakitokea Moshi mkoani Kilimanjaro kwenda Tunduma.

Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, Dk. Athumani Mkanachi, alisema wahamiaji hao haramu wana asili ya Ethiopia na Somalia, walikuwa wakitokea Moshi kwenda Tunduma wakiwa wanatafuta mpaka mwingine ili waendelee na safari yao.

"Kwa namna hasa walivyohesabika wako vijana 51 wenye asili ya Kihabeshi (Ethiopia) na Kisomali. Vijana hawa wote hawawezi kuzungumza Kiswahili, Kiingereza wala Kiarabu, wanazungumza lugha zao za asili. Kwa hiyo sasa mtihani na sisi hatuzijui kwa hiyo hatuwezi kuwa na mazungumzo wala mawasiliano," aliseema Dk. Mkanachi.

"Kwa maelezo ya askari, gari hili lilikuwa likitokea Moshi na kwa ruti ambayo dereva walikubaliana ni kufika Iringa na baadaye alisema ilikuwa kwenda Tunduma kwa lengo la kutafuta mpaka,"alisema Mkanachi.

Alisema baada ya askari polisi kulisimamisha gari hilo, waligundua makosa mbalimbali yakiwamo madeni na walipotaka kulichunguza kwa kina ndipo dereva aliyejulikana kwa jina la Mgosi, alikuwa akionyesha hali ya kukataa kukaguliwa jambo ililowapa wasiwasi askari kutaka kujua ndani kuna nini ndipo walipogundua kuna wahamiaji haramu.

Mkuu wa Wilaya alilipongeza Jeshi la Polisi eneo la Bereko kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kiuzalendo kwa kukataa rushwa na kuwadhibiti wahamiaji hao.

Pia alieleza kusikitishwa kuona baadhi ya Watanzania ndio vinara wa kusafirisha binadamu wenzao kama mizigo na kutoa wito kwa wananchi wa Kondoa hususani vijana kujishughulisha na kazi za uzalishaji ndani na hata nje ya nchi kama kilimo.

Alionya kwamba serikali ipo makini kuwashughulikia watu wenye tabia za kuwaingiza nchini wahamiaji haramu kama hao.

Naye Ofisa Uhamiaji Wilaya ya Kondoa, Mrakibu Msaidizi Zabibu Mkobe, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo.

Alisema wahamiaji hao haramu 51, wakiwamo Watanzania wawili ambao ni dereva aliyejulikana kwa jina la Mgosi na fundi wa gari hilo aliyejulikana kwa jina la Jafari Iddi, wamepelekwa jijini Dodoma kwa ajili ya taratibu zingine za kisheria.





# Mbaroni tuhuma mauaji kisa kugombea chakula

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linamshikilia kijana mmoja na wengine watatu wanasakwa kwa tuhuma za mauaji katika matukio matatu tofauti mkoani hapa.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ulrich Matei, alimtaja anayeshikiliwa kuwa ni Masele Lige (30) mkazi wa kijiji cha Ujerumaji wilayani Chunya.

Alisema kijana huyo ambaye ni mchimbaji wa dhahabu katika kijiji hicho, anatuhumiwa kumuua mchimbaji mwenzake, Mhojamadale Mihambo (30) na kwamba chanzo cha mauaji hayo ni kugombea chakula.

Kamanda Matei alisema tukio hilo la mauaji lilitokea Desemba 24, mwaka huu, majira ya saa 12:30 alfajiri. Alisema mtuhumiwa kwa kushirikiana na mwenzake ambaye ametajwa kwa jina moja la Clement walimuua Mihambo kwa kumpiga na sululu maeneo mbalimbali ya mwili.

"Inasemekana kwamba watuhumiwa walikuwa wanamtuhumu Mihambo kuwa alikuwa hatoi michango ya chakula lakini alikuwa anakula. Lakini huyu Clement alitoroka baada ya kutekeleza mauaji hayo," alisema Kamanda Matei.

Pia Kamanda Matei alisema jeshi hilo linaendelea na msako mkali wa kumtafuta Clement huku likiendelea kumhoji Lige na kwamba upelelezi ukikamilika atafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

Katika tukio la pili, Kamanda Matei alisema jeshi hilo linamtafuta mtu mmoja aliyejulikana kwa jina moja la Lole, Mkazi wa Kiwanja wilayani Chunya kwa tuhuma za kumuua Samwel Chisunga (19) mkazi wa wilaya ya Mbozi mkoani Songwe.

Alisema Lole alitekeleza unyama huo Desemba 25, mwaka huu, wakati wa sherehe za Krismasi saa 11:00 alfajiri katika kijiji cha Mlimanjiwa kwa kumshambulia Chisunga marehemu kwa fimbo katika maeneo mbalimbali ya mwili na kusababisha kifo.

Matei alisema baada ya tukio hilo, mtuhumiwa alitokomea kusikojulikana na jeshi hilo linaendelea na msako huku wananchi wakiombwa kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa endapo watamwona.

Katika tukio la tatu, Kamanda Matei alisema jeshi linamsaka Sombwile Mwakisambwe mkazi wa kijiji cha Ikolo wilayani Kyela kwa tuhuma za kumjeruhi Paulina Mwaikupa (41) mkazi wa kijiji hicho kwa kumshambulia na kitu chenye ncha kazli.

Alisema tukio hilo lilitokea Desemba 25, mwaka huu, saa 5:00 usiku na kwamba chanzo cha tukio hilo ni kwamba mtuhumiwa alitaka kumbaka Paulina kwa kumvamia nyumbani kwake na baada ya kushtukiwa na majeruhi kupiga kelele za kuomba msaada, ndipo mtuhumiwa aliamua kumshambulia kwa kumpiga na kitu chenye ncha kali.



Mbunge wa Mbeya Mjini ambaye ni Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akizungumza na wananchi wa Kata ya Iziwa alipotembelea kukagua miradi ya maendeleo ikiwamo elimu na barabara. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wakulima wafunzwa mabadiliko tabianchi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA mkoani Mbeya wameshauriwa kupanda mazao yanayokomaa kwa muda mfupi ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yanaikumba dunia kwa sasa.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, Dk. Tulole Bucheyeki, alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa mipango mbalimbali ya kilimo.

Alisema kwa sasa kuna tatizo la uhaba wa mvua ambalo lilishatangazwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) lakini kutokana na uelewa mdogo wa baadhi ya wakulima bado wanapanda mazao yanayokomaa muda mrefu.

Aliwataka pia kulima mazao yanayovumilia ukame ili endapo mvua itakata mapema mazao hayo yavumilie na kustahimili kwa muda ambao utakuwa umebaki.

"Sisi hapa tumebuni teknolojia mbalimbali za kilimo na tuna teknolojia karibu 81, lakini sasa hivi tumeanza kuzitoa ambazo zinahusu masuala ya mabadiliko ya tabianchi. Kuna mazao ambayo tunawashauri wananchi wazalishe zaidi ikiwamo mihogo na viazi," alisema Dk. Bucheyeki.

Alisema kwa wakulima ambao wanalima mahindi wanatakiwa kupanda mbegu ambazo zinakomaa kwa kipindi cha chini ya miezi minne ambazo alisema baadhi zimezalishwa na kituo hicho.

Mtaalamu wa Utafiti wa Mahindi TARI Uyole, Leonard Sabula, alisema wanaendelea kutoa elimu ya kilimo kwa wananchi wa mikoa yote ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambao baadhi wanakwenda kwa vikundi na wengine wanafuatwa kwenye maeneo yao.

Sabula aliwataka wananchi waendelee kutembelea kituo hicho kwa ajili ya kupata elimu ya kununua mbegu ambazo zinastahimili ukame kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

# Umeme kupelekwa vituo vya afya na maji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA), imesema inakusudia kupeleka umeme kwenye vituo vya afya na vyanzo vya maji kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma hizo vijijini.

Imeelezwa kuwa mpango huo ni sehemu ya mikakati ya serikali ya kukabiliana na maambukizi ya wimbi la nne la virusi vya corona kwa kuhakikisha kunakuwa na maji ya kutosha kwa ajili ya kunawa na matumizi mengine kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Wajumbe wa Bodi ya REA walieleza hayo jana walipofanya ziara ya kukagua utekelezaji wa mradi wa ujazilizi wa umeme kwenye vijiji kata ya Utengule - Usongwe katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani hapa.

Mjumbe wa Bodi hiyo, Florian Haule, alisema kuna mpango wa serikali wa kuhakikisha kila kituo cha kutolea huduma za afya kinakuwa na umeme na kwenye vyanzo vya maji ili huduma hizo ziwe za uhakika.

Alisema kwa sasa serikali inapambana kuhakikisha huduma za umeme na maji zinakuwapo kwenye vituo vya kuhudumia wagonjwa wa corona huku akisema watafunga transfoma kwenye vyanzo vya maji.

Pia alisema nishati hiyo itasaidia dawa kutunzwa kiurahisi kutokana na baadhi ya dawa hizo kuhitaji huduma hiyo ili zihifadhiwe kwa usalama zaidi.

"Kuna mradi ambao wafadhiri wetu wametuahidi kuwa unatakiwa uanze, utafanyika kwenye zahanati, vituo vya afya na kwenye vyanzo vya maji kwa lengo la kupambana na ugonjwa wa corona," alisema Haule.

Kwa sasa, alisema wanapambana kuhakikisha mradi huo wa ujazilizi unatekelezwa kwa ufanisi katika maeneo yote ya vijiji ili wananchi waendelee kuitumia huduma hiyo kwenye shughuli zao zikiwamo za kiuchumi.

Baadhi ya wananchi wa maeneo yaliyokuwa yamerukwa wakati wa awamu ya kwanza na ya pili ya usambazaji wa umeme, waliishukuru serikali kwa kuwapelekea huduma hiyo kwa maelezo kuwa kuna waliokuwa wanaipata mbali na makazi yao.

Japhet Mbewa, mkazi wa kitongoji cha Mwanjelwa katika kijiji cha Utengule, alisema walikuwa wanashindwa hata kununua mashine za kusaga kutokana na kukosa nishati hiyo licha ya kuwa na uchumi mzuri.

Alisema wanawake walikuwa wanalazimika kwenda kusaga maeneo ya Mbalizi au kutumia gharama kuwatumia vijana wanaoendesha pikipiki, maarufu kwa jina la bodaboda, kupeleka mahindi kwenda kusaga.

"Kama unavyoona hapa kwetu sasa hivi vijana wameanzisha biashara. Kuna wengine wanachomelea, wengine wanachajisha simu na wengine wanakodisha CD. Kwa hiyo tunaona hii ni fursa nzuri ambayo serikali imetuletea," alisema Mbewa.

Naye Philemon Mwalyego ambaye ameanzisha shughuli ya kuchomelea, alisema kwa muda mrefu alikuwa na ujuzi wa fani ya kuchomelea, lakini alikuwa anashindwa kuanzisha biashara hiyo kwa sababu ya kukosekana kwa umeme.



## Sababu ya meli kutotia nanga

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MELI kubwa ya kitalii ya Le Bellot iliyobeba zaidi ya watalii 69 imeshindwa kutia nanga katika Bandari ya mkoani Pemba kutokana na udogo wa eneo.

Watalii hao 69 kutoka nchi mbalimbali za Ulaya walitembelea kisiwa cha Pemba na kupata fursa ya kujionea mandhari ya kisiwa hicho kwa kutembelea mashamba ya karafuu, ya viungo na magofu ya kale.

Ofisa Mdhamini wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba, Zuhura Mgeni, alisema ujio wa watalii hao ni fursa muhimu ya kukifungua kisiwa cha Pemba kuingia katika ramani ya utalii.

Alisema hiyo ni sehemu ya mikakati ya Serikali ya Zanzibar kuona Zanzibar inapokea idadi ya watalii hadi kufikia 500,000 miaka mitano ijayo.

Lengo la Kamisheni ya Utalii kwa upande wa Pemba ni kuongeza watalii hadi kufikia 150,000 kwa mwaka kutoka watalii 35,000.

"Kisiwa cha Pemba kimeanza kufunguka katika utalii kutokana na juhudi kubwa za kutangaza sekta hiyo kimataifa. Matarajio yetu sasa ni kupokea watalii na kufikia malengo ya watalii 150,000," alisema.

Mkurugenzi wa kampuni ya East Africa Holidays inayoratibu safari ya meli hiyo, Duwe Lazaro, amethibitisha ujio wa meli hiyo na kusema kisiwa cha Pemba kinayo nafasi kubwa ya kutangaza sekta ya utalii duniani kutokana na mazingira yake ya kuvutia pamoja na fukwe nzuri.

"Meli hiyo imeanza safari zake katika kisiwa cha Seycheles kutoka Mauritius na kuelekea Pemba hadi Afrika ya Kusini ambapo matarajio yetu sasa kisiwa cha Pemba kitafunguka katika sekta ya utalii na uwekezaji zaidi," alisema.

# Waziri ataka siri mafanikio Mapinduzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MOJA ya mafanikio makubwa baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 ni kutungwa kwa Katiba ya kwanza iliyotungwa mwaka 1979, imeelezwa.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa wizara yake, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Dk. Khalid Salum Muhammed, alisema lengo kuu la kuwa na katiba hiyo ya mwaka 1979 na kuanza kutumika rasmi 1980 ni kuendeleza Mapinduzi, kudumisha uhuru na umoja, kuleta haki, usawa, heshima na utu.

Dk. Khalid alisema katiba hiyo inaendelea hadi sasa kutumika licha ya marekebisho mbalimbali na ndiyo iliyowezesha kuanzishwa kwa Baraza la Wawakilishi lililozinduliwa rasmi Januari, 1980 na Rais wa Awamu ya Pili, Aboud Jumbe Mwinyi.

Alisema katika jitihada za kudumisha Muungano ambao ni moja ya tunu za taifa , viongozi katika ngazi mbalimbali za pande mbili za Muungano wamekuwa wakikutana tangu mwaka 1964 ili kuondoa kero zinazojitokeza.

"Mwaka 2006 katika Awamu ya Nne ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ulianzishwa mfumo maalumu wa kuwa na vikao vya majadiliano kati ya viongozi wa Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa nia ya kuzifanyia kazi kero zilizojitokeza katika Muungano," alisema.

Waziri huyo alisema tangu mwaka 2006 kero 27 ziliwasilishwa na kujadiliwa na Kamati ya pamoja na SMT na SMZ ya kushughulikia kero za Muungano na kati ya hizo, 19 zimeshapatiwa ufumbuzi na changamoto 8 zinaendelea kuchukuliwa hatua za utatuzi. Alizitaja kero zinazoendelea kufanyiwa kazi ni mgawanyo wa mapato yatokanayo na hisa za SMZ zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki pamoja na faida ya Benki Kuu, malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili, usajili wa vyombo vya moto, na ongezeko la gharama za umeme kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwenda lile la Zanzibar (ZECO).

Kero zingine, kwa mujibu wa waziri, ni mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha, mkataba wa mkopo wa fedha za mradi wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume na uingizaji wa sukari inayozalishwa Zanzibar katika soko la Tanzania Bara.

Pia alisema miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana kwa kuanzishwa kwa Baraza la Wawakilishi ni kufanyika marekebisho ya 10 ya Katiba ya Zanzibar kulikowezesha kuwa na Serikali ya mfumo wa Umoja wa Kitaifa. Alisema pia kuongezeka kwa uwajibikaji wa serikali unaotokana na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuhoji mambo mbalimbali yanayohusu wizara na taasisi za serikali tokea kuanzishwa kwa Baraza la Wawakilishi mwaka 1980 hadi mwaka huu jumla ya miswada ya Sheria 453 imeshapitishwa.

Waziri huyo alisema tokea Mapinduzi ya mwaka 1964, Zanzibar imepiga hatua kubwa katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi na kukuza demokrasia pamoja na kuongeza ushiriki wa wananchi katika maamuzi yanayohusu nchi yao.



Baadhi ya wadau wa kilimo cha viungo wakiwa katika kiwanda cha Makonyo Wawi Pemba wakichuma maua ya mlangi langi ambayo hutumika kwa ajili ya kutengeneza mafuta na manukato mbalimbali. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wajumbe PAC wapongeza makusanyo kidijitali

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAJUMBE wa Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) ya Baraza la Wawakilishi, wameelezea kufurahishwa na juhudi zilizochukuliwa na serikali ya Zanzibar kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji mapato ambao utaziba mianya iliyokuwa ikivujisha mapato.

Mwenyekiti wa PAC, Juma Ali Khatib, alisema hayo jana wakati akifunga mafunzo kwa wajumbe wa kamati hiyo kwa ajili ya kujenga ufanisi wa ufuatiliaji wa majukumu ya kamati kuhusu matumizi ya fedha za serikali.

Khatib alisema kilio kikubwa cha muda mrefu cha PAC kilikuwa kuwapo kwa matumizi sahihi ya fedha za serikali.

Alisema matumizi ya mashine za kielektroniki katika matumizi ya fedha za serikalini ndiyo njia pekee ya kuziba mianya ambayo watumishi wasio waaminifu walikuwa wakiitumia, hivyo kulikosesha fedha taifa.

"PAC tumefurahishwa na kuanza kwa mchakato wa matumizi ya mfumo wa kielektroniki ambao tunaamini utaziba mianya yote ya upotevu wa fedha," alisema.

Mjumbe wa PAC, Asha Abdalla Mussa, alisema wamefaidika na mafunzo ambayo yatakuwa mwongozo katika utekelezaji wa majukumu ya ufuatiliaji wa fedha za serikali katika mashirika ya umma na serikali.

Alisema mafunzo hayo sasa yatawajengea uwezo katika kufuatilia kasoro mbalimbali za mashirika ya umma katika masuala ya makusanyo ya fedha.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Jamal Kassim Ali, alisema taasisi zote za serikali zinazokusanya mapato na fedha zimeanza rasmi kutumia mfumo huo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA INAUZWA

NYUMBA INAUZWA MOROGORO MJINI MASIKA MIL. 100. NI NZURI KWA BIASHARA, INA VYUMBA KUMI NA NNE. KWA MAWASILIANO **PIGA SIMU NAMBA**: **0745 222 312 / 0715 768 811.**

## KIWANJA KIANUZWA.

KIWANJA KIANUZWA KISUSURU JKT KIWANJA KIPO KISUSURU JKT SEGEREA UKUBWA SQM 2252 KINA HATI BEI MILIONI 55, **KWA MAWASILIANO: 0786 857523 AU 0655 857523**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**MOHAMEDSADIQ SAMEER MARASHI** anatangaza kupotea kwa Hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE202255** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam **27 SEPTEMBER 2019.**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi:
**DAR/SEL/RB/588948/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

IBRAHIM YERIKO MBILINYI anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili T 197 DHV aina ya M/ROSA. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: MKB/RB/278/2021.

**LAND DISPUTE COURTS (THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL)**
**FORM NO. 28**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA TUNDURU**
**MAHALI: TUNDURU**
**MAOMBI NO: 2/2021**
**FATUMA SELEMANI KIUTILA……MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
- **NEEMA KASILI NYANGWINDA**
- **MOSES ELIAS SHIREKA….MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA: NEEMA KASILI NYANGWINDA NA MOSES ELIAS SHIREKA WA TUNDURU**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 24 mwezi wa 1 mwaka 2022 saa 2:00 asubuhi mbele ya Mheshimiwa **H. LUKEHA** Mwenyekiti wa baraza. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya baraza siku hiyo bila kukosa.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa baraza hili leo tarehe 27 mwezi 12 mwaka 2021.

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**NGWITO CHRISTOPHER MAGITA**
Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC. 105 BVM.**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya Jeshi la Polisi.
**KAH/RB/2048/2021.**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MOROGORO**
**SHAURI LA MADAI NA.22/2021**
**JUMA LUKINDA MAJEGELO……MDAI**
**DHIDI YA**
**PATHEC LIMITED……………MDAIWA**

**KWA: PATHEC LIMITED**

**POPOTE ULIPO**

Mahakama hii inakufahamisha kwamba Mdai amefungua madai dhidi yako.
Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 17/01/2022 Saa 2:30 asubuhi na untakiwa kuwepo,au kuwakilishwa kisheria pamoja na kuleta utetezi wako dhidi ya madai haya.
Zingatia kwamba kutofika kwako tarehe hiyo,shauri litaanza kusikilizwa bila ya wewe kutaarifiwa tena,na maamuzi kutolewa.
Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 28 mwezi 12 mwaka 2021.

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT COURT OF MVOMERO**
**AT MVOMERO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 01 OF 2021**

**In the Matter of the Estate of the Late WENDELIN JOHN MAGUBIKA**
**AND**
**IN THE MATHER OF AN APPLICATION FOR PROBATE AND LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**MPEKA WENDELIN MZUANDA…………….APPLICANT**

**GENERAL CITATION**
**(Made under rule 75 of the Probate Rules,G.N.-No.369/1963)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 11th day of JAN….. 2022
**Dated at Mvomero this 20 day of 12…2021**

Resident Magistrate

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**GEORGINA RAPHAEL WAPILILA**
Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 686 DQG,** Trailler **No, T. 658 DQD.**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake, Taarifa ya Jeshi la Polisi.
**KAH/RB/634/2021.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**BAHATI MOSHI MASABILE**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA SCANIA YENYE NAMBA ZA USAJILI T 655 BYY YENYE CHASSIS NO 5108616 NA ENGINE NO 6232122
KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI
TAARIFA YA POLISI
MWANZA / RB/ 9833/2021

**IN THE HIGH COURT OF UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**TEMEKE HIGH COURT SUB – REGISTRY**
**(ONE STOP JUDICIAL CENTRE)**
**AT TEMEKE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO. 72 OF 2021**
**In the Matter of the Estate of the Late**
**MENDRADY AMBROSE SAKAYA**
**and**
**In the Matter of an Application for Letter of Administration By**
**TASIANA JOHN SHAYO……………….PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant letters of administration is made to the above-named petitioner. Objections to the grant should be filled on or before 13th day of January, 2022.
**Dated at this 27th day of December, 2021.**

DEPUTY REGISTRAR

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Marekani yaiunga mkono Somalia

**Mogadishu,** SOMALIA

MAREKANI imesema jaribio la kumsimamisha kazi Waziri Mkuu wa Somalia, Mohammed Hussein Roble, lilikuwa la kustusha na kwamba inaunga mkono juhudi zake za uchaguzi wa haraka na wa kuaminika.

Idara ya Masuala ya Afrika ya Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani, ilisema katika ukurasa wake wa Twitter juzi, kwamba iko tayari kuchukua hatua dhidi ya wale wanaozuia njia ya amani ya Somalia.

Rais Mohamed Abdullah Mohamed alisema amesitisha mamlaka ya Roble kwa tuhuma za ufisadi, hatua ambayo waziri mkuu aliitaja kuwa jaribio la mapinduzi na kuzidisha mzozo wa madaraka kati ya viongozi hao wawili.

**Jaribio la kusimamishwa kwa Roble, linatisha na tunaunga mkono juhudi zake za uchaguzi wa haraka na wa kuaminika, ofisi hiyo ilisema.**

"Jaribio la kusimamishwa kwa Roble, linatisha na tunaunga mkono juhudi zake za uchaguzi wa haraka na wa kuaminika, ofisi hiyo ilisema. Pande zote lazima zijiepushe na vitendo na kauli za kuongeza mvutano," ilisema Marekani.

Rais Mohamed alimshutumu Roble kwa kuiba ardhi inayomilikiwa na Jeshi la Kitaifa la Somalia (SNA) na kuingilia uchunguzi wa wizara ya ulinzi.

Wakati huo huo, washirika wa Somalia wameelezea wasiwasi wao, kuhusu kuongezeka kwa mvutano kati ya rais wa nchi hiyo na waziri mkuu, huku makundi pinzani ya askari wenye silaha nzito yakiweka doria katika maeneo ya mji mkuu Mogadishu.

Wanajeshi watiifu kwa Waziri Mkuu, Mohammed Hussein Roble, walijikusanya karibu na ikulu ya rais, siku moja baada ya Rais Mohamed Abdullah Mohamed, maarufu kama Farmajo, kutangaza kutimuliwa kwa Roble, ambaye alimtuhumu kwa kufanya njama ya jaribio la mapinduzi.

Waangalizi wa kimataifa na washirika, ukiwamo ujumbe wa Umoja wa Mataifa wa Kulinda Amani nchini Somalia (AMISOM), Marekani, Umoja wa Ulaya (EU) na Umoja wa Mataifa (UN), walitoa taarifa juzi usiku, wakielezea wasiwasi kuhusu mzozo huo.

Taarifa hiyo iliwataka viongozi wa Somalia, kuyaweka mbele maslahi ya nchi, kuituliza mivutano ya kisiasa inayoongezeka, na kujiepusha na uchochezi au matumizi ya nguvu ambavyo vinaweza kuhujumu amani na utulivu. **VOA**

## Makundi ya Kiislamu yapinga sare ya shule India

**Kerala,** INDIA

MZOZO umezuka kwenye Jimbo la Kerala, Kusini mwa India baada ya shule ya serikali, kuwaruhusu wanafunzi wasichana kuvaa suruali.

Manafunzi Sringi CK, alisubiri akiwa kwenye kituo cha basi kwenda shuleni, akiwa amevaa sare yake mpya, alipata pongezi kutoka kwa mwanamke ambaye hakumfahamu hatua iliyofanya ajisikie vizuri.

"Mwanadada mmoja aliniambia nilikuwa nadhifu sana na kwa kweli nilifarijika sana," msichana huyo mwenye umri wa miaka 17 wa darasa la 11 katika shule ya serikali ya wasichana kwenye mji wa Balussery, aliiambia BBC.

Sringi alipowasili lango la shule, alikumbana na waandamanaji waliokuwa wamezuiwa na polisi ambao walikuwa wakilalamika kwamba, wasichaana hawastahili kuvaa suruali na shati kama wavulana.

Kabla ya mabadiliko hayo, wanafunzi wa kike walivaa kanzu ndefu za kitamaduni, suruali zilizolegea na koti za kufika kiunoni.

Mwalimu Mkuu, Indu R, aliiambia BBC kuwa mwaka uliopita wasichana ambao kwa sasa wako darasa la 12, walipendekeza kuruhusiwa kuvaa sare sawa na za wavulana.

Alisema aliona uzito kwenye pendekezo hilo, wengi wa wanafunzi huvaa jeans na koti kama wasichana wengine popote pale duniani na koti la kufika kiunoni, halikuwa bora kwa hali ya hewa yenye unyevunyevu ya Kerala.

"Kwa hivyo tulijadili suala hili na walimu kisha tukaita mkutano wa walimu na wazazi. Wengi walikubali kwa hivyo tukaamua kubadilisha," Indu alisema.

"Lakini ni wasichana wachache wamebadilisha," aliongeza.

Indu alituma picha kwa BBC za kundi la wanafunzi wakiwa na sare zao mpya, wakipiga selfii wakicheka na kuruka kwa furaha. **BBC**




Wafanyakazi wakiwa kwenye stendi mpya ya usafiri wa umma wa treni wakati ikizindua kuanza kwa safari zake, jijini Dakar, nchini Senegal, juzi. Mradi huo wa treni una kilomita 40, utasafirisha abiria 115,000 kwa siku kutoka Dakar hadi Diamniadio, umegharimu dola bilioni 1.3. **PICHA: REUTERS**

## Ethiopia yahuzunishwa kuondolewa AGOA

**Addis Ababa,** ETHIOPIA

ETHIOPIA imesema haijafurahishwa na uamuzi wa Marekani wa kuiondoa kwenye mkataba wa AGOA.

Mkataba huo unatoa nafasi kwa mataifa ya Afrika kusafirisha bidhaa nchini Marekani, bila ya kutozwa ushuru.

Taarifa ya Wizara ya Biashara Ethiopia, imekuja baada ya utawala wa Rais Joe Biden, Desemba 23 kuiondoa Ethiopia kunufaika na mpango huo wa AGOA.

Marekani ilisema, hatua hiyo imetokana na mgogoro uliopo katika Jimbo la Tigray.

Ethiopia imetoa wito kwa Marekani, kufikiria upya juu ya uamuzi wake.

Taarifa ya wizara iliongeza kwamba nchi hiyo ya pembe ya Afrika, inatekeleza mipango inayolenga kupata utulivu, amani, na maridhiano ya kisiasa.

Marekani pia imeziondoa Guinea na Mali kutika mkataba huo wa AGOA, kuanzia Januari Mosi, 2022. **DW**

## Rais wa Brazil adai hatampa chanjo bintiye

**Brasilia,** BRAZIL

RAIS wa Brazil, Jair Bolsonaro, amesema hatampa chanjo bintiye, mwenye umri wa miaka 11 dhidi ya ugonjwa wa COVID-19.

Hatua hiyo ni mwendelezo wa msimamo wake hasi wa kupinga chanjo, ambao umekosolewa na wataalamu wa afya ya umma, na hata kuathiri wafuasi wake wa kisiasa.

Kiongozi huyo wa mrengo wa kulia, aliongeza kwamba Waziri wa Afya Brazil, Marcelo Queiroga, ataeleza Januari 5 mwakani, jinsi ambavyo nchi hiyo, itaendesha kampeni yake ya chanjo dhidi ya corona, kwa watoto wa miaka mitano hadi 11, ambayo iliidhinishwa mapema mwezi huu.

"Watoto wamekuwa hawafi kwa njia ambayo inahalalisha chanjo kwa watoto," aliwaambia waandishi wa habari katika Jimbo la Kusini, Santa Catarina. **VOA**

# SBL KUENDELEA KUCHANGIA MAENDELEO YA MICHEZO

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti Breweries Limited (SBL), imesema itaendelea kuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha na kuchangia sekta ya michezo hapa nchini ambayo inaajiri Watanzania wengi kupitia shughuli mbalimbali zilizoko ndani ya sekta hiyo.

**Kwa mujibu wa Meneja Chapa Mwandamizi wa SBL, Wankyo Marando, Serengeti imekuwa ni mdau mkubwa wa maendeleo ya michezo na imekuwa ikifadhili michezo mbalimbali ikiwamo soka, riadha na mchezo wa gofu.**

Wankyo alisema SBL inatambua mchango wa michezo na kwamba kupitia Chapa ya Serengeti imekuwa mstari wa mbele kuchangia maendeleo katika sekta hiyo.

Ni kupitia udhamini wa Bia ya Serengeti Lager, timu ya Taifa 'Taifa Stars' iliweza kufuzu mashindano makubwa kabisa barani Afrika ya Mataifa ya Afrika (AFCON) yaliyofanyika nchini Misri mwaka 2019. Taifa Stars ilifuzu mashindano hayo ikiwa ni miaka 39 tangu ifuzu kwa mara ya mwisho.

Kabla ya kufuzu mashindano hayo makubwa barani Afrika, SBL kupitia kinywaji chake cha Serengeti Lager, ilisaini mkataba wa miaka mitatu na TFF ambapo ilitoa kiasi cha Sh. bilioni 2.1 kuidhamini Taifa Stars katika kipindi cha miaka mitatu, udhamini ambao ulikuwa na mafanikio makubwa kwa timu hiyo.

Oktoba mwaka 2020, Bia ya Serengeti Premium Lager (SPL) iliingia makubaliano na kusaini mkataba na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), kwa ajili ya kuidhamini Taifa Stars kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.

Wakati wa kutiliana saini mkataba huo, Rais wa TFF, Wallace Karia, alinukuliwa akisema SBL kupitia Chapa ya Serengeti imekuwa ni mfano wa kuigwa katika kuchangia maendeleo ya michezo na kuyataka makampuni mengine kuiga mfano.

Mkataba huo unaogharimu Sh. bilioni tatu za Kitanzania, umesainiwa baada ya ule wa awali uliosainiwa mwaka 2017, kufikia ukomo katikati ya mwaka huu huku timu ikijivunia mafanikio mengi katika kipindi cha udhamini huo.

SBL kupitia Bia ya Serengeti Lite, pia imekuwa mdau mkubwa wa soka la wanawake kwani imekuwa mdhamini wa kwanza na wa pekee kwa ligi ya wanawake tangu ianzishwe hapa nchini. SBL pia imekuwa ikisaidia michezo mingine ikiwamo gofu na riadha.




Rais wa TFF, Wallace Karia, akizungumza wakati shirikisho hilo lilipotiliana saini mkataba na Kampuni ya Bia ya Serengeti, Septemba 2020, ambapo SBL kupitia bia yake ya Serengeti Premium Lager imekuwa mdhamini rasmi wa Timu ya Taifa Stars hadi sasa. **PICHA: MAKTABA**

## *Simba kung'oa beki kisiki Coastal Union*

**Na Saada Akida**

WAKATI Simba wakiingia kambini kujiandaa dhidi ya Azam FC, kuna taarifa kwamba beki wa Coastal Union, Hance Masoud, yupo katika mipango ya kujiunga na 'Wekundu wa Msimbazi' hao, imefahamika.

Kikosi cha Simba juzi, Jumatatu kiliendelea na programu ya mazoezi kwa kuanzia gym na leo kitaingia kambini rasmi kuanza kuziwinda pointi tatu muhimu dhidi ya Azam FC, lengo likiwa ni kutetea ubigwa wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Taarifa kutoka chanzo cha uhakika ndani ya klabu hiyo, ni kwamba beki huyo wa Coastal Union ameingia katika rada za Simba kwa ajili ya kuimarisha timu yao kulingana na ripoti ya Kocha Mkuu, Pablo Franco.

Mtoa habari huyo alisema licha ya uongozi kuwa kimya, lakini tayari kamati ya usajili inayoongozwa na Mwenyekiti wake, Kassim Dewji, imeshafanya vitu vyake kimyakimya.

Alisema tayari uongozi upo katika mchakato wa usajili huku benchi la ufundi linaloongozwa na Pablo wakiendelea na maandalizi kwa ajili ya mchezo wao dhidi ya Azam FC.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha Pablo alisema wachezaji wameingia kambini kwa ajili ya mchezo dhidi ya Azam FC ambao anaamini utakuwa na ushindani mkubwa. Alisema ligi imekuwa na ushindani mkubwa na hakuna timu iliyokuwa nyepesi kwao kwa sababu zote zimejiandaa vizuri kwa ajili ya kutafuta pointi tatu.

"Nina imani na wachezaji wangu kupambana kutafuta pointi tatu katika kila mechi, licha ya kuwapo kwa changamoto ya ungojwa kwa wachezaji wetu, lakini walifanya vizuri katika mechi iliyopita dhidi ya KMC FC, Tabora.

## KMKM yajiandikia rekodi Ligi Kuu Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya KMKM imeweka rekodi yake kwa kumaliza mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Zanzibar kwa kutofungwa baada ya juzi kuhitimisha mzunguko wa kwanza kwa kutoka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Mlandege.

KMKM ambayo imecheza michezo 15, imeshinda tisa huku ikipata sare sita katika mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo yenye timu 16, na hiyo ni mara ya kwanza kwake kumaliza mzunguko wa kwanza bila kupoteza.

Kwa matokeo hayo KMKM inakwenda mapumziko ya dirisha dogo ikiwa bado kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kwa kufikisha alama 33.

Akizungumza na gazeti hii jana, Kocha wa KMKM, Ame msimu huku akiwa na furaha, alisema haikuwa kazi rahisi kupata matokeo yenye mafanikio katika Ligi Kuu ambayo imejawa na ushindani zaidi.

Alikiri kwa kusema kuwa timu yake ilizidi kuimarika kadri walivyoshuka dimbani ikilimganishwa na walipoanza ligi ambapo yalijitokeza mapungufu kadhaa ya kiuchezaji.

## Yosso Boys yapania ubingwa Mapinduzi Cup

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Yosso Boys imesema imejipanga kuhakikisha inanyakuwa ubingwa wa Kombe la Mapinduzi msimu huu kwenye michuano hiyo inayotarajiwa kuanza rasmi mapema Januari 02, mwakani.

Yosso Boys ambayo itaanza kampeni zake za kusaka ubingwa huo Jumanne ijayo dhidi ya Namungo FC, Kundi lao la A pia linazijumuisha Azam FC na Meli 4 City.

Akizungumza na gazeti hili mwanzoni mwa wiki hii, Kocha wa timu hiyo, Abrahaman Abdallah, alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha ndoto hiyo inatimia na kuwapa raha mashabiki wanaofuatilia michuano hiyo.

Alisema kupata fursa ya kushiriki mashindano hayo haimaanishi waishie kwenye ushiriki tu, bali wapo katika kuhakikisha wanatoa ushindani wa kweli na hata kuunyakuwa ubingwa huo.

"Tumejipanga kufanya makubwa katika mashindano haya makubwa, tupo katika kupambana ili lengo la kunyakuwa ubingwa wa kombe hili litimie. Kwa mara ya kwanza tunacheza mashindano haya hivyo haimaanishi ndio tushindwe kupambana,"alisema.

## ZISIKUPITE

### SPURS WAONGOZA KWA KASSIE

KLABU ya Tottenham wanaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsajili kiungo wa kati wa Ivory Coast, Franck Kessie, 25, ambaye mkataba wake na AC Milan unakamilika msimu wa majira ya joto. Arsenal na Manchester United pia wanamtaka lakini Spurs tayari wamefanya mazungumzo na kambi ya Kessie. ***(Express)***

### HOWE HAMTAKI DELE

KOCHA wa Newcastle United, Eddie Howe hataki kumnunua kiungo wa kati wa Tottenham Hotspur, Dele Alli, 25, kwa vile anataka kuimarisha sehemu nyingine za timu yake kwenye dirisha la Januari. ***(Football Insider)***

### RAPHINA AKARIBIA CHELSEA

CHELSEA wako tayari kushindana na Liverpool kujaribu kumsajili winga wa Brazil, Raphinha, 25, kutoka Leeds United msimu wa majira ya joto. ***(Sport Italia, via Express)***

### KUBADILISHWA NA JAMES

REAL Madrid wanavutiwa na beki wa kulia wa Chelsea na England, Reece James, 22, na wanaweza kujaribu kuwajaribu 'The Blues' kwa kumpa winga wa Ubelgiji, Eden Hazard kama sehemu ya mkataba wowote. ***(El Nacional)***

### MAITLAND-NILES RASMI ROMNA

KIUNGO wa Arsenal na England, Ainsley Maitland-Niles, 24, anakaribia kukamilisha usajili wa mkopo na AS Roma. ***(Mirror)***

### WAJIPANGA KWA HAALAND

KIPAUMBELE cha Real Madrid ni kumsajili mshambuliaji wa Norway, Erling Braut Haaland, 21, kutoka Borussia Dortmund msimu ujao, lakini klabu hiyo ya Hispania inamtazama mshambuliaji wa Fiorentina, Dusan Vlahovic, 21, kama mbadala wake. ***(El Nacional)***

### ODOI ATAKIWA NAPOLI

WINGA wa Chelsea na England, Callum Hudson-Odoi, 21, analengwa na Napoli, ambayo inanolewa na kocha wa zamani wa 'Blues' hao, Maurizio Sarri. ***(Tuttosport, via Football Italia)***

### COUTINHO HUYOOO ARSENAL

BARCELONA wanataka kumwachia huru mchezaji wa Brazil, Philippe Coutinho, 29 na chaguo analopendelea mchezaji huyo ni kwenda Arsenal. ***(Sport)***

### BEI YA BOTMAN YATAJWA

KLABU ya Lille ya Ufaransa, inataka angalau euro milioni 30 ikiwa watalazimika kumuuza mlinzi wa Uholanzi, Sven Botman, 21. ***(Tuttomercatoweb)***

### BELLOTTI KUTIMKA TORINO

MSHAMBULIAJI wa Italia, Andrea Belotti, 28, yuko tayari kuondoka Torino wakati mkataba wake na timu hiyo ya Serie A utakapokamilika msimu wa majira ya joto, huku AC Milan, Napoli na Fiorentina zikimwania mchezaji huyo. ***(Calciomercato, via Football Italia)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# DEST AINGIA NDANI YA RADA ZA USAJILI ARSENAL

●●● Chelsea na Bayern Munich pia wanasemekana kufuatilia hali hiyo huku ofa zikitayarishwa kuelekea...

**LONDON,** England

KLABU ya Arsenal imeripotiwa kwamba, wamemtambua mlinzi wa Barcelona, Sergino Dest kama moja ya malengo yao ya uhamisho mwaka 2022.

Licha ya kuwachezea wababe hao wa Catalunya mechi 57 za mashindano yote kwa kipindi cha miezi 18 iliyopita, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, anadaiwa kuwapo sokoni kwa uhamisho.

**Barcelona inatajwa kuwa tayari kupokea ofa kutokana na masuala yao ya kifedha yanayoendelea, na mchezaji huyo wa kimataifa wa Marekani hana shaka na klabu za kuhamia dirisha lijalo.**

Kwa mujibu wa NBC Sports, Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta anavutiwa na mchezaji huyo na yuko tayari kufikiria mbinu ya kumpata.

Licha ya 'Washikabunduki' hao kuwa na machaguo ya kutosha upande wa kulia, wanaweza kuwa tayari kutengana na moja ya chaguo zao za ziada ili kuwa na Dest.

Chelsea na Bayern Munich pia wanasemekana kufuatilia hali hiyo huku ofa zikitayarishwa kuelekea mwisho wa mwaka huu.









# BAYERN HAWAMTAKI HAALAND

**MUNICH,** Ujerumani

MKURUGENZI Mtendaji wa Bayern Munich, Oliver Kahn amethibitisha kwamba, wababe hao wa Bavaria hawatakuwa kwenye kinyang'anyiro cha kuwania saini ya Erling Haaland mwaka ujao.

Mabingwa hao wa Bundesliga ni moja kati ya timu zinazotajwa zaidi kuisaka saini ya mchezaji huyo wa Borussia Dortmund wakati kipengele chake cha kuachiwa kitakapoanza kutumika msimu wa joto.

Bayern wanakabiliwa na sintofahamu kuhusu mustakabali wa mshambuliaji nyota wa sasa Robert Lewandowski, lakini Kahn hatarajii mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway kuondoka hivi karibuni.

Kahn akizungumza na Suddeutsche Zeitung alisema, "Tunaye Robert Lewandowski. Atafunga mabao 30 au 40 zaidi kwa miaka kadhaa ijayo, hivyo hatumhitaji Erling Braut Haaland."

Kutokana na hali hiyo, Manchester United, Barcelona, Paris Saint-Germain, Real Madrid na Manchester City wanapunguziwa ushindani kumpata Haaland, huku timu hizo zikisemekana zinataka kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway mwaka ujao.

Haaland amefikisha mabao 76 katika michezo 75 pekee ya Dortmund kwenye mashindano yote, ikijumuisha mabao 19 kutoka mechi 16 za msimu wa 2021-22.



# Madrid kumbadilisha Hazard na James

**MADRID,** Hispania

KLABU ya Real Madrid imeamua kufanya dili na Chelsea endapo wanataka kumrejesha Eden Hazard katika viunga vya Stamford Bridge kwenye kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili.

Real Madrid wako tayari kumtoa Hazard kurudi Chelsea kama sehemu ya makubaliano ya kumnunua Reece James, kwa mujibu wa Jarida la El Nacional.

Taarifa ndani ya klabu hiyo zinaeleza wapo tayari kufanya usajili mpya wa beki wa kulia kusaidiana na Dani Carvajal, na kocha Carlo Ancelotti amemtaka Rais Florentino Perez kumnunua James.

Perez anatarajia kusu-
luhisha matatizo
kwa pamoja kwa k
James na kumrudis
ard katika klabu
msajili kama sehe
makubaliano.

Ingawa
Abramovich ang
kumrejesha Hazar
London, lakini ha
kwa gharama ya
wa wachezaji ny
timu yake kuondok

LIVE IN PLAY

# BURIANI GENERAL DEFAO

**Na Dennis Fussi**

• Akiwa Dar alikosa nauli ya kurudi Congo, akapewa 'lift' na ATCL



MWANAMUZIKI mahiri wa muziki wa Rhumba kutoka Jamhuri ya Watu wa Congo (DRC), Le General Defao Matumona, amefariki dunia akiwa nchini Cameroon, baada ya kuugua kwa muda mfupi.

Defao mwenye umri wa miaka 62, alifariki Jumatatu, Desemba 27, katika Hospitali ya Laquintinie huko Douala, Cameroon, ambako alikuwa amelazwa hospitali. Wanamuziki Ferre Gola na Fally Ipupa walikuwa miongoni mwa watu wa kwanza kuwasilisha salamu zao za rambirambi, wakielezea kifo chake kuwa ni pigo kwa Afrika.

Defao alizaliwa Desemba 31, mwaka 1958 katika jiji la Kinshasa huko Congo na kupewa majina ya Mutomona Defao Lulendo. Alikuwa ni mwanamuziki mwenye kipaji cha kutunga na kuimba kwa sauti nyembamba na nyororo.

Defao alianza kujishughulisha na muziki mwaka 1976, akiwa katika bendi ya Orchestra Suka Movema kabla ya kuhamia Fogo Stars. Mwaka 1978 alienda kupiga muziki katika bendi ya Korotoro huko Somo, Magharibi mwa Congo.

Alikuwa mmoja kati ya wanamuziki waliounda bendi mpya ya Grand Zaiko Wawa mwaka 1981, ikiongozwa na mpiga gitaa mashuhuri Pepe Felix Manuaku. Katika kile kilichoitwa mbinu za kujitafutia maisha, Defao aliungana na mwanamuziki Ben Nyamabo kuunda kikosi kipya cha Choc Stars.

Bendi hiyo ya Choc Stars na Orchestra Shakara Gagna Gagna, zilikuwa chini ya uongozi wa Jeanpy Wable Gypson, zilimfanya Defao kuwa maarufu kwa mara ya kwanza kitaifa.

Akiwa na wanamuziki kina Ben Nyamabo, Debaba, Carlito, Bozi Boziana na Djuna Djunana, bendi ya Choc Stars ikajizolea umaarufu mkubwa kupitia tungo zao.

Defao kwa kawaida alicheza sambamba na wanenguaji wake, ambapo huwa kivutio kikubwa cha wapenzi na mashabiki wake akicheza mitindo mbalimbali ukiwamo ule wa 'Ndombolo' pasipo kuchoka.

Ilipofika mwishoni mwa mwaka 1990, aliiacha bendi hiyo ya Choc Stars, akiwa na madhumuni ya kuunda bendi yake na akafanya hivyo kwa kuunda bendi yake iliyopewa jina la Big Stars.

Katika bendi hiyo alipiga muziki kwa kushirikiana na mwimbaji mwingine Djo Poster, aliyetokea katika bendi ya Grand Zaiko.

Defao aliomwongeza katika safu ya wanamuziki mpiga solo chipukizi, Jagger Bokoko, ambaye alitokea kuwa kipenzi chake kikubwa.

Bendi ya Big Stars ilikuwa na wanamuziki wengi wenye uwezo mkubwa wa kutengeneza muziki.

Kulikuwa na waimbaji kina Djo Djo Bayenge, Debleu Kinanga na Adoli Bamweniko na kwa upande wa wapiga magitaa, kulikuwa na Mogus aliyekuwa akilicharaza gitaa la solo, gita la besi likiungurumishwa na Guy wa Nzambi.

Katika kipindi cha miaka mitano ya bendi ya Big Stars, Defao alionyesha ubunifu uliomletea mafanikio makubwa baada ya kufyatua album zisizopungua 17. Kati ya hizo, sita ziliingia katika soko la Ulaya mwaka 1995.

Mifarakano katika sehemu za kazi huwa hazikosi na Big Stars iliteteteka kwa kipindi kifupi baada ya kuondoka Djo Djo Bayenge na kumuacha Defao akiwa kiongozi wa bendi hiyo.

Umaarufu wa General Defao ulizagaa maeneo mengi Afrika Mashariki na Kati kwenye miaka 1990. Wapenzi na mashabiki wake waliulinganisha umaarufu wake na ule wa wanamuziki akina Papa Wemba, Koffi Olomide, Bozi Boziana na Kester Emeneya.

Nyimbo kama Georgina, Fammilie Kikuta, Nadine, Bana Kongo, Oniva na Filie zilimpatia umaarufu mkubwa. Defao alilivunja kundi zima la Big Stars mwaka 2000 wakiwa katika Jiji la Kinshasa na yeye akaamua kwenda 'kutanua' katika Jiji la Paris, Ufaransa.

Lakini akiwa katika jiji hilo, alirekodi albamu ya Nessy de London, akiwashirikisha wanamuziki nyota waishio katika jiji hilo la Paris. Wanamuziki hao walikuwa akina Nyboma Mwandido, Luciana de Mingongo, Wuta Mayi, Ballou Canta na Deesse Mukangi, walioshirikiana na Defao kufanya onyesho kubwa lililo wavutia watu wengi.

Katika hali isiyokuwa ya kawaida, Defao baadaye akawa kimya katika anga ya muziki. Hali hiyo yasemekana kuwa ilitokana na sintofahamu ya kisiasa nchini mwake iliyosababisha kufungiwa kupiga muziki huko kwao Congo. Defao alifika nchi za Afrika ya Mashariki ikiwamo Tanzania katika ziara yake ya hapa nchini iligubikwa na matatizo lukuki mwaka 2000.

Baada ya kumaliza kufanya maonyesho kadhaa, Defao alizidiwa akili na 'Mapromota' waliomleta, matokeo yake alifikia hadi kukosa fedha ya kujikimu pamoja na kulipia Visa yake. Nguli huyo 'alifulia' hata nauli ya kumrejesha kwao Congo hakuwa nayo.

Bahati njema ilikuwa upande wake kwa kuwa alifanikiwa kurejea kwao baada ya kupewa 'lift' katika ndege ya Shirika la Ndege la Tanzania (ATC), aliyokuwa ikizindua safari zake kati ya Dar es Salaam na Lubumbashi nchini DRC.

"Kimya kingi kina mshindo mkuu" usemi huu ulijionyesha wazi kwa gwiji hilo lililosubiriwa na wapenzi kwa kipindi kirefu hadi mwaka 2006, ndipo alipotoka na albamu yake mpya yenye Lebo ya Nzombo le Soi. Baada ya miaka minne mingine alifyatua CD yake yenye Lebo ya Pur Encore mwaka 2010. Mwaka 2012 Defao kwa bahati nzuri alirudi ulingoni akiwa na album ya The Undertaker.


SPORTPESA APP

BET LEO UWE MILIONEA





MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 29 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 2306 | AFC Leopards vs KK Homeboyz | 4.50 | 3.45 | 1.83 |
| 15:00 | 2365 | Kariobangi Sharks vs FC Talanta | 1.90 | 3.12 | 3.94 |
| 15:00 | 3160 | Fatih Karagumruk vs Bodrumspor | 1.56 | 3.72 | 5.21 |
| 15:00 | 3377 | Bandari vs Ulinzi Stars | 1.87 | 3.09 | 4.16 |
| 15:00 | 3790 | Mbarara FC vs Gaddafi FC | 1.92 | 3.50 | 3.95 |
| 15:00 | 3992 | Vihiga Bullets FC vs Sofapaka | 7.60 | 4.50 | 1.42 |
| 15:00 | 4060 | Police FC (UGA) vs Bright Stars | 1.98 | 3.40 | 3.85 |
| 15:15 | 4116 | AL Kawkab vs AL Sahel SC | 3.30 | 3.40 | 2.17 |
| 16:00 | 1892 | AE Larissa vs SKODA Xanthi | 3.03 | 2.89 | 2.36 |
| 16:10 | 2040 | Al-Shamal vs Al Rayyan SC | 5.21 | 4.34 | 1.48 |
| 16:30 | 5013 | Sanat Naft Abadan vs Aluminium Arak | 3.32 | 2.93 | 2.18 |
| 17:00 | 1918 | Adana Demirspor vs Osmanlispor | 1.20 | 6.15 | 9.60 |
| 17:00 | 5347 | ATK Mohun Bagan vs FC Goa | 1.79 | 3.57 | 3.81 |
| 17:35 | 1940 | Al Qadisiyah vs Hajer Club | 2.40 | 3.45 | 2.85 |
| 18:00 | 1746 | RS Berkane vs Athletic Youssoufia | 1.83 | 3.17 | 4.23 |
| 18:00 | 4285 | Heartland FC Owerri vs Akwa Starlets FC | 1.55 | 3.42 | 6.16 |
| 18:00 | 4593 | Remo Stars vs Nasarawa United | 1.67 | 3.29 | 5.03 |
| 18:00 | 4649 | Enyimba vs Rivers United FC | 1.52 | 3.53 | 6.37 |
| 18:00 | 5052 | Akwa United vs Gombe United FC | 1.12 | 6.56 | 18.34 |
| 18:20 | 2174 | Al Gharafa SC vs Al-Sailiya SC | 1.86 | 3.56 | 3.56 |
| 18:20 | 2414 | Al Ahli Doha SC vs Lekhwiya SC | 6.73 | 5.19 | 1.32 |
| 18:30 | 1039 | Viseu vs Nacional Madeira | 2.84 | 3.18 | 2.39 |
| 18:30 | 2026 | Goeztepe vs Samsunspor | 1.72 | 3.46 | 4.33 |
| 18:30 | 4213 | Leixoes vs Mafra | 2.74 | 3.13 | 2.50 |
| 20:00 | 5689 | Famalicao vs Belenenses | 1.76 | 3.49 | 4.53 |
| 20:15 | 1035 | Difaa El Jadidi vs Rapide Oued Zem | 1.55 | 3.71 | 5.39 |
| 21:00 | 4297 | Fenerbahce vs Afjet Afyonspor | 1.15 | 6.79 | 11.63 |
| 22:00 | 3168 | Vitoria Guimaraes vs Boavista | 1.65 | 3.75 | 4.94 |
| 22:30 | 3148 | Jeunesse Sportive Soualem vs Olympique Safi | 2.01 | 3.04 | 3.67 |
| 22:30 | 4202 | Chelsea vs Brighton | 1.43 | 4.50 | 7.20 |
| 22:45 | 1045 | Wigan vs Fleetwood Town | 1.56 | 4.02 | 5.29 |
| 22:45 | 1554 | Sutton United vs Colchester | 1.86 | 3.39 | 4.02 |
| 22:45 | 1658 | Ipswich vs Wycombe | 2.24 | 3.33 | 2.99 |
| 22:45 | 1830 | Hartlepool vs Tranmere | 2.34 | 3.19 | 2.95 |
| 22:45 | 1951 | Coventry vs Millwall | 2.00 | 3.38 | 3.53 |
| 22:45 | 2203 | Oxford Utd vs AFC Wimbledon | 1.72 | 3.77 | 4.31 |
| 22:45 | 2410 | Blackpool vs Middlesbrough | 3.10 | 3.25 | 2.22 |
| 22:45 | 2464 | Blackburn vs Barnsley | 1.65 | 3.78 | 4.81 |
| 22:45 | 2649 | Morecambe vs Crewe | 2.23 | 3.34 | 3.00 |
| 22:45 | 2987 | Sheffield Utd vs Hull City | 1.53 | 3.92 | 5.88 |
| 22:45 | 3333 | Swindon Town vs Stevenage | 1.93 | 3.39 | 3.73 |
| 22:45 | 3436 | Crawley Town vs Bristol Rovers | 2.39 | 3.23 | 2.84 |
| 22:45 | 3750 | Rochdale vs Port Vale | 2.25 | 3.25 | 3.05 |
| 22:45 | 4110 | Plymouth vs Portsmouth | 2.28 | 3.44 | 2.85 |
| 22:45 | 4710 | MK Dons vs Cheltenham | 1.86 | 3.48 | 3.92 |
| 22:45 | 4735 | Shrewsbury vs Accrington | 2.24 | 3.24 | 3.09 |
| 22:45 | 5022 | Airdrieonians vs Queens Park | 2.57 | 3.25 | 2.57 |
| 22:45 | 5479 | Rotherham vs Lincoln | 1.39 | 4.61 | 6.87 |
| 22:45 | 5677 | Barrow vs Oldham | 1.92 | 3.39 | 3.78 |
| 23:15 | 3043 | Brentford vs Manchester City | 14.11 | 6.35 | 1.20 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


mawili
kumleta
sha Haz-
waliyo-
emu ya

Roman
gefurahi
rd jijini
taki aje
mmoja
ota wa
ka.

# Michezo

Jumatano Desemba 29, 2021

Nipashe

Dest ndani ya rada za Arsenal UKURASA 21

# CAF yamleta tena Chama Simba SC

## Kisinda naye yumo, Hitimana aachia ngazi, kuanza na Asec Mimosas...

**Faustine Feliciane na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Soka Afrika (CAF), limewarejesha wachezaji wa zamani wa Simba na Yanga, Mzambia Clatous Chama (pichani) na Mkongomani Tuisila Kisinda, kuwavaa wawakilishi hao pekee wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu.

**Hiyo ni baada ya jana CAF kuipanga Simba kundi moja kwenye hatua ya makundi na Klabu ya RS Berkane ya Morocco wanayoichezea kwa sasa Chama na Kisinda.**

Katika droo iliyochezeshwa jana jijini Cairo, Misri, mbali na RS Berkane na Simba, timu hizo zimepangwa Kundi D pamoja na Asec Mimosas ya Ivory Coast na US Gendarmerie Nationale (USGN) ya Niger.



Droo hiyo imeshuhudiwa TP Mazembe ya DR Congo ikipangwa Kundi C na timu za Coton Sports ya Cameroon, Al Masry ya Misri na AS Otoho ya Congo.

Kundi B zipo timu za Orlando Pirates ya Afrika Kusini, JS Saoura ya Algeria, Al Itihad ya Libya na mshindi kati ya timu ya JS Kabylie na Royal Leopards ya Congo watakutana na miamba hiyo kwenye kundi hilo.

Kundi A kwenye michuano hiyo litazikutanisha timu za Pyramids FC ya Misri, CS Sfaxien ya Tunisia, Zanaco ya Zambia na Ahly Tripoli ya Libya.

Kwingineko kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, wababe wa Simba msimu huu, Jwaneng Galaxy wamepangwa Kundi C na klabu za CR Belouizdad ya Morocco, Etoile du Sahel ya Tunisia na Esparance de Tunis ya Tunisia.

Jwaneng ndio iliyowaondoa Simba kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu kwa faida ya bao la ugenini baada ya matokeo ya jumla kuwa 3-3 kabla ya Simba kuangukia michuano ya Kombe la Shirikisho.

Kundi A la michuano hiyo litazikutanisha Klabu ya Al Ahly ya Misri, Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, Al Hilal na Al Merrikh za Sudan.

Kundi B lina timu ya Raja Casablanca ya Morocco, Horoya ya Guinea, Es Setif ya Algeria na Amazulu ya Afrika Kusini.

Nyota wa Tanzania, Simon Msuva ataiongoza timu yake ya Wyadad Casablanca ya Morocco kwenye Kundi D linalozijumuisha Zamalek ya Misri, Petro de Luanda na Sagrada Esperanca za Angola.

Hatua hiyo ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho inatarajiwa kuanza Februari mwakani.

Ligi ya Mabingwa michezo yake ya kwanza itapigwa kati ya Februari 11 na 12. Kwa upande wa Kombe la Shirikisho Simba itaanzia nyumbani dhidi ya Asec mimosas Februari 13.

Katika hatua nyingine, Kocha Msaidizi wa Simba, Thierry Hitimana, ameliambia Nipashe kuwa hatakuwa tena sehemu ya benchi la ufundi la timu hiyo baada ya pande hizo mbili kufikia makubaliano ya kusitisha mkataba.

"Kuanzia sasa sitakuwa sehemu ya benchi la ufundi la Simba baada ya pande zote mbili kuafikiana kusitisha mkataba," alisema Hitimana huku akifunguka kuwa muda wowote ataondoka nchini kuelekea kwao, Rwanda.

## HATUA YA MAKUNDI

### Kombe la Shirikisho Afrika

**KUNDI A**
- AL AHLY TRIPOLI
- CS SFAXIEN
- PYRAMIDS
- ZANACO

**KUNDI B**
- AL- ITTIHAD
- ORLANDO PIRATES
- JS SAOURA
- JS KABYLIE/ R. LEOPARDS

**KUNDI C**
- AL MASRY
- COTON SPORT
- OTOHO D'OYO
- TP MAZEMBE

**KUNDI D**
- ASEC MIMOSAS
- RS BERKANE
- SIMBA SC
- USGN



# Yanga kumnasa kipa wa Mtibwa

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

BAADA ya dili la kipa Metacha Mnata wa Polisi Tanzania kuonekana kusuasua kwenda Yanga, klabu hiyo sasa ipo kwenye mazungumzo na kipa chipukizi wa Mtibwa Sugar, Abutwalib Msheli.

Uongozi wa Mtibwa Sugar umekiri hatima ya kipa wao huyo kujiunga na Yanga itajulikana leo baada ya kukutana na kupitia ofa iliyofika mezani kutoka kwa klabu ya Yanga.

Hatua hiyo ya Yanga kuamua kusajili kipa mwingine katika dirisha hili dogo, ni kutokana na mlinda mlango wao namba moja, Diarra Djigui kuitwa timu ya Taifa ya Mali, kwenda kuitumikia kwenye michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) itakayoanza Januari 6, mwakani nchini Cameroon.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mtendaji Mkuu wa Mtibwa Sugar, Sabri Abuubakar, alisema wamepokea barua kutoka Yanga ikihitaji huduma ya kipa wao, Msheli ila hawajatoa majibu hadi bodi itakapokutana leo.

Alisema mbali na barua ya Yanga, lakini watajadili ombi la kipa huyo la kusitisha mkataba wake na kuwa mchezaji huru.

"Tumepokea barua kutoka Yanga ikimuhitaji kipa wetu huyo, ambaye bado ana mkataba na Mtibwa Sugar wa mwaka mmoja na nusu, hatujawajibu Yanga wala mchezaji mwenyewe kuhusu kusitisha mkataba, tunasubiri bodi itakapokutana.

"Baada ya mechi yetu ya leo (jana) dhidi ya Coastal Union, bodi itakaa kuangalia madai ya kipa huyo pamoja na barua ya Yanga, kutokana na kwamba tuko katika hali mbaya kwenye ligi, hivyo hatima ya maamuzi ya kuondoka Msheli yatakuwa baada ya kikao hicho," alisema Sabri.

Lakini kwa upande wa Klabu ya Yanga kupitia kwa Ofisa Habari wake, Hassan Bumbuli, alisema watatangaza majina ya wachezaji ambao imewasajili wakati wowote kuanzia leo, na imeweka utaratibu maalum wa kuwatambulisha.

"Hivi sasa hatusemi tu tumemsajili mchezaji fulani, tuna utaratibu tumeweka jinsi ya kuwatambulisha, ndivyo tatakavyofanya," alisema.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >